



KIPIIMO CHA VYOMBO VYA HABARI BARANI AFRIKA

Uchambuzi wa ndani ya nchi wa mandhari
ya vyombo vya habari barani Afrika

TANZANIA 2019



KIPIMO CHA VYOMBO VYA HABARI BARANI AFRIKA

Uchambuzi wa ndani ya nchi wa mandhari
ya vyombo vya habari barani Afrika

TANZANIA 2019

Imechapishwa na:

Friedrich-Ebert-Stiftung (FES)

fesmedia Africa

Windhoek, Namibia

Simu: +264 61 417523

Barua pepe: info@fesmedia.org

Tovuti: www.fesmedia-africa.org

© Kazi hii imeidhinishwa chini ya the Creative Commons' Attribution-NonCommercial – ShareAlike 2.5 Licence.

ISBN: 978-99945-77-84-2

Mauzo au matumizi ya kibashara ya machapisho yote ya Friedrich-Ebert-Stiftung (FES) na yale ya Taasisi ya Vyombo vy'a Habari Kusini mwa Afrika (MISA) yamezuiliwa; isipokuwa kwa idhini ya kimaandishi kutoka kwa FES na MISA.

Kipimo cha Vyombo vy'a Habari Barani Afrika, ambacho kwa lugha ya Kiingereza kinajulikana kama '*The African Media Barometer* (AMB), ni kipimo cha kimtazamo. Matokeo, tafsiri na mahitimisho yanayowasilishwa ni yale yanayotolewa na wanajopo wanaotokana na asasi za kiraia na taasisi za vyombo vy'a habari kwa lengo la kutathmini vyombo vy'a habari; na hivyo haimaanishi kwamba ndio mtazamo na maoni ya *fesmedia* Africa, Friedrich-Ebert-Stiftung (FES) Taasisi ya Vyombo vy'a Habari Kusini mwa Afrika (MISA).

CONTENTS

SUMMARY	6
ENEO LA 1	10
Uhuru wa kujieleza, ukiwemo uhuru wa vyombo vya habari, unalindwa na kukuzwa kikamilifu	
ENEO LA 2	28
Mandhari vyombo vya habari, pamoja na vyombo vipyta vya habari, inaonesha mtawanyiko, uhuru na uendelevu	
ENEO LA 3	40
Sheria ya matangazo ni wazi na huru; vyombo vya umma vimebadilishwa na kuwa vyombo halisi vya umma	
ENEO LA 4	47
Vyombo vya habari vina viwango vyajuu vya weledi	
GRAFU KULINGANISHA	56
NINI KIFANYIKE	60

Kipimo cha Vyombo vya Habari Barani Afrika

Kipimo cha Vyombo vya Habari Barani Afrika (AMB) ni tathmini yakinifu na kamilifu; na mfumo wa upimaji wa mazingira ya kitaifa ya vyombo vya habari katika bara la Afrika. Tofauti na tafiti nyingine zinazohusu vyombo vya habari au vipimo vya vyombo vya habari, AMB ni tathmini rejeshi yenye kuzingatia vigezo vya ndani ya nchi vinavyotokana na Mikataba na Maazimio ya Afrika kama vile Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza Afrika la mwaka 2002 liliotolewa na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu. Zana za utafiti huu ziliundwa kwa ushirikiano kati ya fesmedia Africa, ambao ni mradi wa vyombo vya habari wa Friedrich-Ebert-Stiftung (FES) barani Afrika, na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) mnamo mwaka 2004.

AMB ni uchambuzi unaolenga kupima hali ya vyombo vya habari katika nchi husika na wakati huohuo kuwa kama nyenzo ya kushawishi uboreshaji wa mazingira ya vyombo vya habari. Matokeo ya utafiti hutolewa kwa wananchi wa nchi husika ili waweze kushawishi maboresho ya hali ya vyombo vya habari kwa kuzingatia Maazimio ya Umoja wa Afrika (AU) pamoja na mifumo ya Kiafrika kama vielelezo. Mapendeleko yanayotolewa kwenye taarifa ya AMB hatimaye yanajumuishwa kwenye tathmini nyinginezo zilizofanyika kwenye nchi zipatazo 20 zenye ofisi za FES Kusini mwa Bara la Afrika, na kujumuishwa pia kwenye jitihada mbalimbali za ushawishi kuhusu vyombo vya habari unaofanywa na taasisi nyingine za vyombo vya habari katika nchi husika kama vile MISA.

Mbinu na mfumo wa utoaji alama

Kila baada ya miaka mitatu hadi minne, jopo la wataalam kati ya 10 na 12 lenye kujumuisha angalau wanahabari watano na wawakilishi watano wa asasi za kiraia hukutana kwa lengo la kutathmini hali ya vyombo vya habari katika nchi zao wenye. Kwa muda wa siku moja na nusu hivi, jopo hilo hujadili mazingira ya vyombo vya habari kwa kuzingatia vigezo 39 ambavyo hutumika kama adidu za rejea. Mjadala na utoaji wa alama hujadiliwa pamoja mshauri elekezi ambaye pia huhariri taarifa ya AMB.

Baada ya kujadili kigezo kimoja, wanajopo huweka alama zao kwenye kigezo husika ambapo huridhiwa kwa kura ya pamoja kwa mujibu wa kielelezo kifuatacho:

- 1 Nchi inakidhi kiashiria
- 2 Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria
- 3 Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria
- 4 Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria
- 5 Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria

Kwa miaka ya 2009, 2013 na 2019, baadhi ya viashiria vilibadilishwa ili kuakisi mabadiliko katika hali ya vyombo nya habari. Matokeo yake ni kwamba, kwenye baadhi ya maeneo, ulinganishi wa viashiria nya taarifa zilizopita hauendani kwa vile kiashiria ama ni ingizo jipya au kimefanyiwa marekebisho makubwa.

Majumuisho ya kipengele kimojakimoja yanagawanywa kwa idadi ya wanajopo ili kukokotoa wastani wa alama kwa kila kiashiria. Wastani wa alama katika kila kiashiria unajumlishwa ili kupata wastani wa alama katika eneo lengwa.

Matokeo

Taarifa ya mwisho ya kitaamuli inatoa muhtasari wa maeleo ya jumla ya mjadala ambao huonesha wastani wa alama kwa kila kiashiria. Majina ya wanajopo hayatambulishwi kwenye taarifa ili kuwaepusha na madhara yanayoweza kuwapata kutokana na michango yao katika mjadala. Taarifa hizi zinaweza kutumiwa kama nyenzo ya kuibua mjadala wa kisiasa kuhusu marekebisho ya mazingira ya vyombo nya habari.

Katika nchi ambazo Kiingereza siyo lugha rasmi, taarifa huchapishwa katika lugha mbili.

Ili kuwafanya AMB, FES na MISA kubakia kama wenyeji wa wanajopo na watoaji wa zana za utafiti, yaliyomo katika majadiliano pamoja na taarifa hubakia kuwa mali ya jopo la wataalam wa ndani ya nchi na hayawakilishi au kuakisi maoni ya FES au MISA.

Kufikia mwishoni mwa mwaka 2019, AMB ilikuwa imeshakamilika kwa mafanikio mara 121 katika nchi 32 za kiafrika, na katika baadhi ya nchi hizo ikawa ni kwa mara ya sita tayari.

Luckson Chipare

Mkurugenzi wa Kanda

Taasisi ya Vyombo nya Habari

Afrika Kusini (MISA)

Windhoek, Namibia

Freya Gruenhagen

Mkurugenzi

fesmedia Africa

Friedrich-Ebert-Stiftung

Windhoek, Namibia



Angalia hapo juu AMB katika nchi 32 (2005-2019)

Vifupisho vya Maneno

AMB:	Kipimo cha Vyombo vya Habari Barani Afrika
BBC:	Shirika la Utangazaji la Uingereza
BRELA:	Wakala wa Usajili wa Biashara
CORI:	Shirikisho la Uhuru wa Habari
CSO:	Muungano wa Taasisi za Kiraia
DED:	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
DIS:	Mkurugenzi wa Idara ya Habari
EACJ:	Mahakama ya Afrika Mashariki
EACSOF:	Jukwaa la Taasisi za Kiraia Afrika Mashariki
FOI:	Uhuru wa Habari
TEHAMA:	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
IFJ:	Shirikisho la Kimataifa la Waandishi wa Habari
JOWUTA:	Umoja wa Wafanyakazi Waandishi wa Habari Tanzania
LGBTQIA+:	Jumuiya ya Wasagaji, mashoga, na watu wenye tabia za jinsia mbili
LHRC:	Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
MCT:	Baraza la Vyombo vya Habari Tanzania
MLDI:	Shirika la Utetezi wa Kisheria kwa Vyombo vya Habari
MISA:	Taasisi ya Vyombo vya Habari kusini mwa Afrika
MUM:	Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro
NBS:	Ofisi ya Taifa ya Takwimu
NEC:	Tume ya Taifa ya Uchaguzi
NGO:	Shirika lisilo la Kiserikali
OUT:	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
SAUT:	Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine Tanzania
SIM:	Moduli ya Utambulisho wa Mtumiaji
TADIO:	Chama cha Taarifa za Maendeleo Tanzania
TAMWA:	Umoja wa Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania
TASWA:	Umoja wa Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania
TBC:	Shirika la Utangazaji Tanzania
TCRA:	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
TEF:	Jukwaa la Wahariri Tanzania
THRDC:	Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania
TMF:	Taasisi ya Vyombo vya Habari Tanzania
TRA:	Mamlaka ya MapatoTanzania
TZS:	Shillingi za Kitanzania
UDSM:	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
UNESCO:	Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni
UTPC:	Umoja wa Kilabu za Vyombo vya Habari Tanzania
US\$:	Dola ya Kimarekani

KIPIMO CHA VYOMBO VYA HABARI BARANI AFRIKA

Tanzania 2019

Muhtasari

Mwaka 2015, Tanzania ilifanya uchaguzi mkuu ambao ulimweka madarakani Rais wa sasa Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Kwa muda mfupi, Rais Magufuli alikubalika na wengi kutokana na jithada zake za kupambana na rushwa ambazo zimesababisha maofisa wengi wa serikali kutolewa katika nafasi zao. Utawala huu mpya pia umechukua hatua madhubuti kuongeza nidhamu katika utumishi wa umma. Hata hiyo, mtindo wa utawala wa Rais Magufuli na hasa kuhusu uhuru wa kujieleza na uhuru wa habari umekuwa chanzo cha madhila makubwa. Kwa kiasi kikubwa, amejimarisha kiutawala na kuhodhi maamuzi ili kujijengea umaarufu; vyama vyaya siasa vyatupinzani vimeminywa, wakosoaji wa serikali wamekuwa wakikamatwa, na haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza imeathirika vibaya. Mambo haya yanayoogofya ni sehemu tu ya mabadiliko katika nyanja nyingi nchini Tanzania katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Ingawa Tanzania ina katiba ambayo imeeleza haki za msingi za kiraia na za kisiasa, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujieleza, haki hizi zimeminywa. Katika kipindi cha miaka mitatu tangu mwaka 2015, sheria kadha wa kadha za vyombo vya habari zilipitishwa, ikiwemo Sheria ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016, ambayo ina mianya na madhaifu mengi yanayominya uhuru wa kujieleza. Sheria hii inaipa serikali mamlaka makubwa juu ya maudhui ya habari na utoaji leseni kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari. Sheria hii pia inaweka adhabu kali, ikiwemo kifungo gerezani, endapo chombo cha habari kitachapisha habari za kuikashfu serikali, uchochezi, au maudhui mengine yasiyozingatia sheria.

Wakati wanajopo wakiendelea na mjadala, mabadiliko ya hivi karibuni ya Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 yanamtaka mtu yejote au taasisi kupata idhini ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kabla ya kutoa takwimu kwa matumizi ya umma. Sheria hii ilibadilishwa katika kipindi cha nusu mwaka wa 2019 na kwa hiyo haizui tena kuchapisha taarifa ya kitakwimu bila kupata ishini ya ya serikali, lakini bado takwimu rasmi zimeendelea kuhitaji kibali cha NBS. Mnamo mwezi Machi, kabla ya mabadiliko ya hivi karibuni, sheria hii ilitumika kufungia gazeti linalomilikiwa na mtu binafsi la *The Citizen* kwa madai kwamba lilichapisha taarifa za uongo, zenyet kuptotosha na za kichochezi. Gazeti hilo lilichapisha habari kuhusu kushuka thamani shilingi ya kitanzania (Tzs) dhidi ya Dola ya Kimarekani (US\$).

Mnamo mwezi Machi 2018, serikali iliweka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (mtandaoni), ambao uliwataka wamiliki wa blogu na waendeshaji wa

mijadala kupitia majukwaa ya mtandaoni kulipa zaidi ya US\$ 900 kwa mwaka kama ada ya kujandidikisha. Kanuni hizi zilitolewa chini ya Kifungu cha 103(1) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2010. Kanuni hizo pia zinatoa mamlaka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania, ambayo ndio msimamizi wa mawasiliano Tanzania, kuondoa habari mtandaoni. Mamlaka haya hayana kinga yoyote dhidi ya matumizi yasiyo ya haki. Mathalan, ada zinazowekwa na kanuni hizo zilisababisha kufungwa kwa muda kwa *Jamii Forum*, ambao ni mtandao maarufu na jukwaa la habari, mwaka 2018. Kanuni hizi vilevile zinawajibisha watumiaji wa mitandao ya kijamii kwa mahudhui ambayo ‘si ya kistaarabu, yenyé kashfa, au yanayoweza kusababisha chuki kwa jamii,’ pamoja na vifungu vingine vyenye utata.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii hali kadhalika wako kwenye hatari ya kushtakiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015, ambayo inazuia, pamoja na mambo mengine, kumtukana Rais mtandaoni. Serikali pia imetishia kuwashtaki watumiaji wa mitandao ya kijamii watakaoshukiwa kueneza ushoga kwa kupitia mitandao ya kijamii; kwa mujibu wa sheria iliyopo sasa, ushoga ni kinyume cha sheria za nchi. Makundi na watetezi wanaotetea haki za wasagaji, mashoga, na watu wenye tabia za jinsia mbili (LGBTQIA+) pia wamekuwa wakinyanyaswa. Mwaka 2018, serikali ilitangaza kuunda kikosi maalum cha doria kwa lengo la ‘kuwasaka’ watu wanaojihusisha na ushoga.

Uhuru wa kukusanyika pia umeminywa na kumekuwepo na zuio la mikutano ya kisiasa na maandamano ya umma tangu mwaka 2016, pamoja na kwamba Katiba inatoa haki hii. Mikusanyiko yote sharti ipate kibali cha polisi na maandamano ya kisiasa yamezuiliwa kwa nguvu zote kwa nyakati tofauti. Kitu pekee kinachoruhusiwa ni mikutano ya kisiasa inayofanywa na wabunge kwenye majimbo yao ya uchaguzi; ambapo kwa kiasi kikubwa kinawapa faida wabunge wanaotokana na chama tawala, Chama cha Mapinduzi -kwa kuwa kina wabunge wengi wanaotokana na majimbo ya uchaguzi. Serikali imeanza kutumia vifungu vyatamani vyatamani ya sheria na sheria ya kikoloni ya watu wasiokubalika ambayo inapiga marufuku uzururaji, ili kuzuia vijana kukaa vijiweni au kukusanyika.

Pamoja na kwamba jitihada zimefanyika kuboresha upatikanaji wa habari, uhalisia wa haki hii umeendelea kuwa changamoto kubwa. Baada ya miaka mingi ya kupigania haki za vyombo vyatamani ya sheria hiyo, kupata habari bado halijawa jambo rahisi.

Ingawa Tanzania ina wigo mpana wa vyombo vyatamani ya sheria, kwa njia ya maandishi, vituo vyatamani ya luminga (TV) na redio, mitandao na blogu, mazingira kandamizi ya kisheria na udhibiti yanaathiri matumizi na uendeshaji wa majukwaa haya ya habari. Aidha, mambo mengine yasiyo ya kisheria yanazuia upatikanaji wa vyanzo vyatamani ya sheria. Bei ya magazeti na bando kwa mfano, vinaathiri upatikanaji wa magazeti na habari za mitandaoni vijijini na kwa watu wasio na uwezo. Kupata matangazo ya kidijitali sasa kunazilazimu familia kununua luminga ya kisasa zaidi au kununua king’amuza.

Ingawa huduma za matangazo (hasa kwa njia ya redio) zinapatikana kwenye sehemu kubwa ya nchi, kuna mawanda finyu sana kwenye vyombo vya habari. Tanzania ni jamii mchanganyiko yenyе makabila zaidi ya 120 pamoja na lugha za kijamii, lakini mchanganyiko huu haujidhihirishi kwenye vyombo vya habari kwa sababu sheria inazua matumizi ya lugha za kijamii kwenye vyombo vya habari. Shirika la utangazaji la taifa -Shirila la Utangazaji Tanzania (TBC), ambalo linatakiwa kuwafikia watu wote, linadhibitiwa vikali na hutumiwa kama kipaza sauti cha serikali au chama tawala, na hivyo kuzima sauti za watu wenye mawazo mbadala.

Sauti za wanawake mara nyingi huzimwa kwenye vyombo vya habari. Kwa mujibu wa mtandao wa GenderLinks, wanaume bado wanatawala kwenye vyombo vya habari Tanzania.¹ Wanawake wanaofanya kazi kwenye vyombo vya habari pia hunyanyaswa kijinsia. Utafiti uliofanywa na *Internews* kuhusu mchango wa wanawake kwenye vyombo vya habari ulionesha kukithiri kwa unyanasaji wa kijinsia kwenye taasisi zote za habari.² Wanawake pia wanazungumziwa vibaya na viongozi wa serikali na vyombo vya habari.

Mazingira ya vyombo vya habari na waandishi wa habari yamedorora kwa kiasi kikubwa katika miaka ya karibuni; na kwa uchache, magazeti manne yamefungiwa tangu mwaka 2017. Sheria kandamizi, matumizi ya adhabu kubwa na kukamatwa bila kushtakiwa ni baadhi ya mambo yanayowakuta waandishi wa habari. Vilevile, mwanahabari Azory Gwanda ametoweuka nyumbani tangu mwezi Novemba 2017. Kabla ya kutweka, alikuwa ameandika makala kadhaa yaliyolezea mauaji ya viongozi wengi wa kimaeneo na maofisa wa polisi. Kutweka kwake kumesababisha hali ya sintofahamu kwa vyombo vya habari. Waandishi wa habari na vyombo vya habari wamelazimishwa kujihariri wenywewe. Hali ya sintofahamu haipo tu kwa vyombo vya habari lakini pia inawapata hata wanajamii. Watu wanaogopa kubadilishana mawazo ya kisiasa kwa uhuru na angalizo hili limeingia pia kwenye mijadala mitandaoni.

Changamoto nyingine kama vile kushuka kwa viwango vya utoaji taarifa, na rushwa kwa ujumla wake pia zinavikibili vyombo vya habari. Kwa mfano, haki na usahihi katika utoaji habari vinazidi kuperomoka kutokana na sababu anuai kama vile mafunzo hafifu, uharakishaji unatokana na hitaji la kwenda na muda na kuondoka kwa wanahabari nguli. Mbaya zaidi, waandishi wa habari wa Tanzania hawalipwi vizuri. Waandishi wengi hawana mikataba ya ajira, na kwa hivyo, hawapati mafao wanayostahili. Kwa kukosa umoja katika kushughulikia kero zao, waandishi wengi hujihusisha na rushwa. Uhandishi wa habari wa bahasha ya kahawia, ambapo waandishi wa habari hupewa bakhshishi ya fedha ili kuandika habari kwa upendeleo au kuzima habari zenye taswira hasi, unazidi kushika kasi nchini.

Pamoja na hali ya kusikitisha ya hali ya kisiasa na vyombo vya habari, bado kuna matumaini. Ingawa taasisi za kiraia zimekuwa zikilalamikia kuongezeka kwa

1 Jambo hili liliibiliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa GenderLinks, Colleen Lowe Morna, kwenye Mkutano wa Kilele kuhusu Jinsia na Upashaji Habari kuhusu Maendeleo Endelevu uliofanyika Tanzania mwaka 2018.

2 Taarifa ya Uchambuzi wa Usawa wa Kijinsia na Ushirikishaji wa Kijamii uliofanywa na FHI 360 kwa ushirikiano na Internews.

mbinyo wa serikali mwaka mzima kwa njia ya vitisho, uchunguzi, ukamataji na sheria kali, taasisi za kiraia Tanzania (CSOs) na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) bado vina nguvu. Mara nydingi asasi za kiraia huungana na kuchagiza mapambano dhidi ya sheria ambazo zinaathiri uhuru wa vyombo nya habari. Muungano wa Haki ya Habari umeweza kuunganisha nguvu ya taasisi kadha wa kadha za kiraia kuongoza mapambano ya kimkakati dhidi ya sheria kandamizi za vyombo nya habari. Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania na Jukwaa la Muungano wa Asasi za Kiraia Afrika Mashariki wanasifika pia kwa kuchukua hatua dhidi ya masahibu ya vyombo nya habari. Mfano wa hivi karibuni ni mapema mwaka 2019 ambapo mashirika matatu yasiyo ya kiserikali Tanzania yalifungua mashtaka dhidi ya Sheria ya Vyombo nya Habari kwenye Mahakama ya Afrika Mashariki (EACJ). Mahakama hiyo iliamua kwamba vipengele anuai nya Sheria ya Vyombo nya Habari vinaminyia uhuru wa vyombo nya habari na uhuru wa kujieleza, na hivyo kuitaka serikali ya Tanzania kuifutilia mbali sheria hiyo.

Tanzania inaelekea kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020. Tangu ilipohama kutoka kwenye nchi ya chama kimoja cha siasa na kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi, Tanzania imekuwa inafanya chaguzi za amani kwa kiasi fulani. Hata hivyo, mgawanyiko wa kisiasa unaozidi kuongezeka hivi sasa unaashiria wasi wasi mkubwa katika chaguzi hizi zinazokuja. Kama ilivyo kwa chaguzi nyingezeo duniani, kuna ongezeko katika matumizi ya wataalam wapotoshaji kwenye mitandao ya kijamii ili kupindisha mawazo na mitizamo huru. Upotoshaji huu unaofanyika kwa njia ya mtandao pamoja na kujitafutia umaarufu wa kisiasa na mabadiliko katika uthibiti unachangia sana kushusha kiwango cha chaguzi huru na za haki ambazo zimeletea Tanzania sifa kubwa katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.

*Mjadala huu ulifanyika kwenye hoteli ya White Sands, Dar es Salaam,
Tanzania Mei 2019.*



ENEO LA 1:

Uhuru wa kujieleza, ukiwemo uhuru wa vyombo vya habari, unalindwa na kukuzwa kikamilifu

1.1 Uhuru wa kujieleza, ukiwemo uhuru wa vyombo nya habari, umeainishwa kwenye katiba na unapewa msukumo na vipengele vingine nya sheria

Kama ilivyo kwa nchi nyingi za kileo, Tanzania inaongozwa kwa mujibu wa katiba, ambayo kimsingi, ndiyo sheria mama. Mnamo mwaka 2011, Tanzania ilianzisha mchakato wa kutunga katiba mpya ambayo ingekuwa na ‘uhalali na maridhiano ya kitaifa zaidi’. Rasimu ya katiba hiyo ilikuwa na mabadiliko makubwa sana kuhusiana na mkataba katи ya umma na viongozi wa serikali: lakini ilipingwa kwa nguvu zote. Vyama nya upinzani na asasi za kiraia zililalamika kwamba, Bunge la Katiba Tanzania halikuwa na uwakilishi sawia na rasimu waliotengeneza haikuzingatia maoni ya upinzani kama vile vipengele vinavyopunguza madaraka ya Rais. Yaliyojiri baadae na kusababisha mchakato huo kusimama ni kwamba tume ya uchaguzi ilisitisha kura ya maoni iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya Katiba mpya ya Mwaka 2015, na kusema rasmi kwamba uandikishaji wa daftari la wapiga kura ulikuwa umechelewa. Wanajopo wa AMB walisema kwamba kurejesha mchakato wa katiba mpya hakuonekani kama kipaumbele cha serikali iliyopo madarakani, ambayo iliingia madarani kwa kupitia uchaguzi uliofanyika baadae mwaka 2015.

Kwa hivyo, Katiba ya Mwaka 1977³ bado ilikuwa na nguvu kisheria wakati wa tathmini ya mwaka 2019 ya hali ya vyombo nya habari Tanzania. Katiba hii inatambua haki na wajibu kadha wa kadha wa raia, ikiwamo haki ya kujieleza. Haki hii imejumuishwa chini ya vifungu kadhaa vinavyohusiana na ‘haki ya uhuru wa utambuzi.’ Kifungu cha 18 cha Katiba ya Tanzania ya Mwaka 1997 kinaeleza kuwa:

Kila mtu (a) ana haki ya kutoa maoni na kueleza mawazo yake; (b) ana haki ya kutafuta, kupata na/au kutoa taarifa bila kujali mipaka ya kitaifa; (c) ana uhuru wa kuwasiliana na uhuru wa kulindwa dhidi ya kuingiliwa mawasiliano yake; na (d) ana haki ya kupewa habari wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu ya kimaisha na shughuli za watu na pia kuhusu masuala muhimu kwenye jamii.

Ni dhahiri kwamba Katiba hii imeshindwa kuwa wazi kuhusu suala la uhuru wa vyombo nya habari. Wanajopo walibaini kwamba baadhi ya sheria zilizotumika wakati wa ukoloni bado zinatumika ambapo inajulikana kwamba kiasilia sheria hizo ni kandamizi. Shukrani ziwaendee mashirika ya haki za vyombo nya habari kwa kuwa mswada mpya wa katiba mpya ulijumuisha vipengele mahsusvi vinavyohusu ‘uhuru wa kupata habari na uhuru wa vyombo nya habari’. Kifungu cha 31 cha katiba mpya kinaeleza kwamba:

³ Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeshafanyiwa marekebisho mara 14s. Marekebisho ya mwisho yaifanyika mwaka 2005. Angalia Utangulizi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(1) Kila mtu ana haki na uhuru wa (a) kutafuta, kupata, na kutoa habari na taarifa; na (b) kuanzisha chombo cha habari na njia nyinginezo za kusambaza habari bila kujali mipaka ya kitaifa.

(2) Vyombo nya habari vitakuwa huru na vitakuwa na (a) haki ya kupata, kutumia na kutoa habari na taarifa wanazopata; (b) jukumu la (i) kutoa habari na taarifa kwa umma; na (ii) kuhestimu na kulinda utu, heshima, uhuru na hadhi ya raia dhidi ya habari na taarifa wanazopokea, kuandaa na kusambaza.

(3) Serikali na taasisi zake, asasi za kiraia na watu binafsi watawajibika kwa kutoa taarifa kwa umma kuhusu shughuli na utekelezaji wa shughuli zao.

(4) Bunge litatunga sheria kwa minajili ya kulinda: (a) haki na uhuru wa vyombo nya habari; na (b) habari na taarifa kwa minajili ya usalama wa taifa, amani, maadili ya umma, haki, heshima na uhuru wa watu wengine.

Pamoja na mtizamo wake chanya, wanajopo wamebaini kwamba uhuru wa vyombo nya habari uliopendekezwa kwenye katiba mpya haukuwa na tija kama katiba mpya itaendelea kufungiwa kwenye makabati- kama hali ilivyokuwa wakati wa kufanya tathmini hii ya hali ya vyombo nya habari kwa Tanzania. Aidha, wanajopo walikuwa na mtizamo usioridhisha kwa ujumla kuhusu kiasi ambacho katiba iliyopo inatoa uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo nya habari:

Kueleza [uhuru wa kujieleza] kwenye katiba ni kitu kimoja, kutoa uhuru huo ni kitu kingine. Kutoa ina maana kwamba hatua zinachukuliwa kuhakikisha kwamba raia wanapata haki hizo. Lakini hali ni tofauti. Kusema kweli, hakuna haki yoyote inayotolewa katika nchi ya Tanzania. [Badala yake] sheria zinazotakiwa kuchagiza haki hizi zimetengenezwa kwa mtindo wa kuzidhoofisha haki hizo.

Katiba yenye pia imeweka mipaka katika kutumia haki hizo na uhuru huo, ikizingatiwa kwamba kifungu cha 30 kinaeleza kwamba haki zinatumwiwa pale tu zinapokuwa hazikiuki haki za watu wengine na maslahi mapana. Na kwa kukazia zaidi, kifungu hicho kinaongezea kwamba vifungu nya katiba vinavyoainisha haki za msingi za binadamu, uhuru na wajibu haviiuzuii serikali kusimamia sheria zilizopo au kutunga sheria nyingine ambazo zinaweza kuathiri haki na uhuru wa raia ulioainishwa kwenye katiba. Kwa mfano, katiba inabainisha kwamba haki, uhuru na wajibu wa raia vinaweza kuingiliwa kwa madhumuni ya:

Kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma hayazuiliwi na matumizi mabaya ya uhuru na haki za watu binafsi;

Kuhakikisha kwamba ulinzi, usalama wa umma, utulivu wa umma, maadili ya umma, afya ya jamii, mipango ya mijini na vijijini, uchimbaji na matumizi ya madini au kuongeza na kuendeleza mali au maslahi mengine yoyote kwa ajili ya kuimarisha maslahi ya umma; kuhakikisha utoaji maamuzi au amri ya mahakama inayofanya au kutolewa katika

mahakama yoyote ya masuala ya madai au ya jinai; kulinda heshima, haki na uhuru wa watu wengine au usiri wa watu wanaohusika katika mashauri mahakamani, kuzuia utoaji wa taarifa za siri, au kulinda heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama; kuzuia uundwaji, usimamizi na shughuli za taasisi na mashirika binafsi nchini; au kitu kingine chochote kitakachofanyika kwa ajili ya kuendeleza au kuhifadhi maslahi ya taifa kwa ujumla.

Kinyume na kanuni inayokubalika kwa ujumla ambayo inachukulia katiba kama sheria mama, wanajopo walisema kwamba inapofika suala la haki na uhuru, Katiba ya Tanzania inapwaya. Walirudia na kunukuu Kifungu cha 30(5) cha Katiba hiyo, ambapo walisema kwamba ni vigumu kudai haki na uhuru wa kikatiba kwa kuwa inawapa majaji mamlaka kuvuka mipaka ya kikatiba panapokuwepo mgongano wa kimaslahi. Kifungu hicho kinaeleza kwamba:

Katika shauri lolote, inapodaiwa kwamba sheria yoyote iliyotungwa au hatua yoyote itakayochukuliwa na serikali au mamlaka nyingine yoyote inavunja au kuminya haki yoyote ya msingi, uhuru na wajibu kama ilivyoelezwa kwenye vifungu vya 12 hadi 29 vya Katiba hii, na Mahakama Kuu ikajiridhisha kwamba sheria au kitendo husika, kwa kadri kwamba inakinzana na Katiba hii, ni batili, au ni kinyume na Katiba hii, Mahakama Kuu, kama ikiona hivyo, au kama mazingira au maslahi ya umma yanahitaji hivyo, badala ya kuamua kwamba sheria hiyo au kitendo hicho ni batili, itakuwa na mamlaka ya kuamua kuipa serikali au mamlaka nyingine inayohusika muda wa kurekebisha kasoro zilizobainishwa kwenye sheria au kitendo husika kwa muda na namna ambavyo Mahakama Kuu itaamua, na sheria hiyo au kitendo hicho kitahesabika kuwa halali hadi pale kasoro hizo zitakapokuwa zimerekebishwa au muda utakaowekwa na Mahakama Kuu utakapokuwa umemalizika, kutegemeana na kipi kinatangulia.

Pamoja na mianya iliyopo kwenye Katiba, wanajopo waliona kwamba vipengele mbalimbali vya sheria vimepitishwa na mara nyingi vinasimamiwa ambavyo vinakiuka vifungu vya Katiba ambavyo vinatoa uhuru wa kujieleza. Baadhi ya sheria mbaya kabisa ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni na Sheria ya Magereza. Baadhi ya sheria hizi zimeibuka hivi karibuni kabisa na mifano mizuri ni Sheria ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016, ambayo kwa mara nyingine imeingiza makosa ya uchochezi na kutoa kashfa, ikiwemo kuwakashfu marehemu. Wanajopo walisema kwamba kiujumla, kuna dalili za kutungwa kwa sheria kandamizi zaidi ambazo zinaweka vagingi kwa watu na taasisi kutumia haki yao ya uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo nya habari. Wakitolea mfano Sheria ya Vyombo vya Habari, mmoja wa washiriki alisema, "Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976, ambayo ilionekana kuwa kandamizi, ilirithiwa na sheria kandamizi zaidi, yaani Sheria ya Vyombo vya Habari. Tuliomba mkate na badala yake tukapewa nyoka."

Kwa muhtasari, washiriki walionesha kwamba pamoja na kwamba Katiba inatambua uhuru wa kujieleza kama haki, inashindwa kuilinda haki hizo, haizungmzii uhuru wa vyombo nya habari na imeacha mianya inayoruhusu kushamiri kwa sheria nyingine ambazo zinawenza kukiuka haki hizo. Katiba

ambayo ingekuwa na mabadiliko chanya, ambayo inatoa uhuru kwa vyombo
nya habari, imefungiwa ndani na hivyo kufifisha matumaini kuleta mabadiliko
kwenye hali ya vyombo nya habari wakati wowote kwa siku za karibuni.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

Wastani wa alama:

2.3

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 2.8; 2008: 2.4; 2010: 2.7; 2012: 2.5; 2015: 2.7

1.2 Haki ya uhuru wa kujieleza inatumiwa na wananchi, wakiwemo waandishi wa habari, bila hofu

Mwaka 2017, Tanzania iliayfungia magazeti manne kwa muda, na hiki kilikuwa kitendo cha aina yake kufanyika ndani ya mwaka mmoja katika historia ya hivi karibuni ya Tanzania. Hatta hii iliongeza idadi ya machapisho yaliyofungiwa kufikia matano katika kipindi cha miaka miwili na ilidhihirisha mwendelezo wa mazingira mabaya na yenye changamoto kwa tasnia ya uhandishi wa habari na uendeshaji wa vyombo nya habari. Hatta hiyo ilifuaatiwa na maonyo na kukumbushia kulikofanywa na Rais kwamba upashaji habari Tanzania unapaswa kuzingatia maadili. Mwezi Oktoba mwaka 2017, Bwana Henry Maina, Mkurugenzi wa Kanda wa Article 19 Eastern Africa, shirika lisilo la kiserikali lenye kujishughulisha na haki za vyombo nya habari, alisema kwamba, 'Kufungiwa kwa magazeti ni hujuma dhidi ya uhuru wa vyombo nya habari nichini na kunadhoofisha wajibu wa vyombo nya habari kama waangalizi katika jamii ya kidemokrasia. Ni habari mbaya kwamba Tanzania inaonekana kurudi nyuma katika dhamira yake ya kutoa uhuru kwa vyombo nya habari kwa kufungia taasisi za habari bila sababu za msingi. Kufungia vyombo nya habari kama hivi kunaweza pia kusababisha waandishi wa habari kuijhariri wenywewe na hivyo kuchagua habari.'⁴

Wanajopo walisema kwamba serikali imetumia sheria kandamizi na mamlaka yake makubwa kukanya uhuru wa kujieleza. Moja katika ya silaha ya hatari kabisa zilizo kwenye mikono ya mamlaka ni sheria mpya ambayo inazua matumizi ya takwimu rasmi bila idhini. Marekebisho ya mwaka 2018 ya Sheria ya Taifa ya Takwimu ya mwaka 2015 inataka idhini ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kabla ya kuchapisha takwimu rasmi; serikali ilidai kwamba marekebisho haya yalihitajika ili kulinda ukweli na uhalisi wa takwimu. Marekebisho haya

⁴ <https://www.article19.org/resources/tanzania-ban-on-newspapers-raises-concerns-for-press-freedom/>.

yamekosolewa na watu na taasisi mbalimbali kwamba ni kinyume na sheria⁵ lakini bado yameendelea kutumika. Mwezi Machi 2019, pamoja na sababu nyinginezo, sheria hii ilitumika kufungia kwa muda gazeti la *The Citizen* kwa kuandika habari bila kibali kuhusu viwango nya ubadilishaji fedha za kitanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani.⁶ Mamlaka zilisema kwamba gazeti hilo lilifungiwa kwa kurudia kutoa taarifa za uongo na za kichochezi. Hata hivyo, mmoja wa wanajopo alisema, ‘Taarifa hizo zilikuwa za kweli. Tatizo ni kwamba uthibitisho wa taarifa hizo haukufanya na NBS’.

Kwa mujibu wa wanajopo, hujuma dhidi ya uhuru wa habari na uandishi wa habari unaanza kwenye matumizi mabaya ya sheria hadi mashambulizi ya ana kwa ana ya kimwili. Kati ya mwaka 2016 na 2017, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambacho ni taasisi isioya kiserikali, kiliorodhesha matukio 17 ya unyanyasaji dhidi ya waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu na matukio mengine mengi dhidi ya raia wengine.⁷ Mwandishi wa habari za kiuchunguzi Azory Gwanda alitoweka mwezi Novemba 2017, na hadi wakati wa kuchapisha taarifa hii hakuna taarifa yoyote kama bado yuko hai. Asasi za kiraia wanakosoa kutokufanyika kwa uchunguzi wa tukio hili. Kwa mujibu wa wanajopo na Article 19 Eastern Africa, Gwanda alikuwa akichunguza matukio ya mauaji yaliyolenga viongozi wa kimaeneo na maafisa usalama, baadhi ya matukio hayo yakidaiwa kufanywa na ‘washambulaji wapanda pikipiki wasiojulikana’, wakati alipochukuliwa na watu wasiojulikana asubuhi ya tarehe 21 Novemba 2017.⁸

Utata unaoneekana wa serikali dhidi ya uhuru wa kujielea umeibua woga. Wanajopo walibainisha kwamba waandishi wa habari na taasisi za vyombo nya habari wamelazimika kujichuja wenyewe na hivyo kuwa waangalifu na kuchagua habari za kuandika kwa sababu hatari ya kuadhidiwa imekuwa kubwa. Mmoja wa washiriki alielezea mazingira ya sasa kama ifuatavyo:

Waandishi wa habari watakuambia kwamba hawako huru. Sasa hivi, kama unataka kupata mafanikio katika uandishi wa habari, ni lazima uimbe nyimbo za kuitukuza serikali au uandike habari zile tu ambazo wale walioko madarakani wanataka kuzisikia. Uandishi wa habari za kiuchunguzi hazina mpango tena Tanzania. Hata kutoa taarifa za matukio kwa sasa ni hatari sana. Kwa mfano, mamlaka ziliweka adhabu ya shilingi milioni 60 (Dola za Kimarekani 27,000) kwa vituo nya luninga

- 5 Angalia: Benki ya Dunia (2018). Taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya Tanzania ya mwaka 2015. Inapatikana mtandaoni kwa anuani hii: <https://www.worldbank.org/en/news/statement/2018/10/02/world-bank-statement-on-amendments-to-tanzanias-2015-statistics-act>. Mara ya mwisho ilipatikana tarehe 20 Mei 2019.
- 6 Angalia gazeti la Daily Monitor (linapatikana mtandaoni kwa anuani hii: <https://www.monitor.co.ug/News/National/Tanzania-bans-Citizen-newspaper/688334-5002850-r04jI4z/index.html>) na CPJ (Inapatikana mtandaoni kwa anuani hii: <https://cpj.org/2019/03/tanzania-citizen-7-day-publication-ban.php>). Taarifa zote mbili zilipatikana tarehe 20 Mei 2019.
- 7 FIDH and LHRC (2017). Tanzania: Uhuru wa Kujielea Mashakani, Joint Situation Note. No 698a. Inapatikana mtandaoni kwa anuani hii: https://www.fidh.org/IMG/pdf/joint_position_note_tanzania_fidh_lhrc.pdf. Mara ya mwisho ilipatikana tarehe 21 Mei 2019.
- 8 Angalia Article 19 East Africa. Linapatikana mtandaoni kwa anuani: <https://www.article19.org/resources/tanzania-concern-grows-missing-journalist-azory-gwanda/>. Mara ya mwisho kupatikana ilikuwa tarehe 20 Mei 2019.

ambavyo vitarusha mikutano inayofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.⁹

Mwaka 2019, taarifa yenye kichwa cha habari *Yearbook on Media Quality in Tanzania 2018: Synthesised Report on Overall Results* (Taarifa ya Mwaka kuhusu Ubora wa Vyombo vyahabari Tanzania 2018: Taarifa Iliyotolewa kuhusu Matokeo ya Jumla) ilionesa kwamba habari za kisiasa kwenye vyombo vyahabari ya Tanzania zilikuwa zimeshuka kwa kwa kiwango kikubwa.¹⁰ Washiriki waliongezea kwa kusema kwamba taarifa za habari ziliikuwa ‘zinatoka kwenye chanzo kimoja kwa kuwa inazidi kuwa vigumu kulinganisha habari au kuwa na taarifa kuhusu vyanzo’. Kwa mujibu wa mawasilisho yao, hata mawaziri na maafisa wa ngazi za juu wa serikali wamekuwa wakikataa kuongea na waandishi wa habari. Washiriki walisema kwamba kwa mazingira haya, habari, uchambuzi na makala yenye kukosoa serikali vyote vimetoweka kwenye magazeti. Pale ambapo bado vipo, ‘lughya ya uwasilishaji imebadilika’, alisema mmoja wa washiriki. ‘Unajua inabidi usome mistari mitatu ya chini ili uweze kuelewa kinachozungumzwa.’

Wanajopo walisema kwamba nje ya vyombo vyahabari na waandishi wa habari, wananchi hawawezi kutoa mawazo yao kwa uhuru. ‘Redio mbao’ ni msemo unaoelezea njia za mawasiliano yasiyo rasmi kama vile mazungumzo ya mitaani ambayo yalikuwa yamekidhiri kwenye mitaa ya Kiafrika, navyo viko kimya. ‘Zamani, watu waliongea habari za siasa wazi wazi nje ya vituo vyahabari kwenye magazeti au kwenye vituo vyahabari kwenye mabasi. Lakini siku hizi, mada imebadilika na kuwa soka au dini’. Baadhi ya wanajopo walisema kwamba hata mijadala kwenye mitandao ya kijamii ilikuwa imedhibitiwa vilivyo, hasa kwa kutumia sheria mpya ambazo zinawawajibisha waendeshaji wa mijadala kwenye mitandao ya kijamii hata kwa habari iliyotumwa na mchangaiji wa kawaida. Baadhi ya washiriki walisema kwamba ilikuwa imekuwa ni kawaida kutolewa kwenye kundi la WhatsApp au Facebook kwa sababu ya kutoa maoni yanayoonekana kuwa na mguso, ‘watu wamegundua kwamba kuna uhuru wa kujieleza lakini hakuna uhuru baada ya kujieleza. [Kutumia haki ya] uhuru wa kujieleza kunategemea unachokisema na ni nani unayemzungumzia.’

Vifungu vyahabari vya zamani vyahabari dhidi ya ‘wahuni na wazururaji’, ambavyo vinaharamisha uzururaji na kukaa bila kazi vimechimbiliwa hivi karibuni na vimeongezewa mkazo. Washiriki walisema hali kama hiyo imeonekana kwenye matumizi ya Sheria ya Watu Wasiokubalika, sheria ya chinichini iliyobakia tangu wakati wa utawala kandamizi wa kiloni. Katika mfano mmoja uliotolewa na mwanaajopo anayejua mkasa huo, wanafunzi wa chuo kikuu kimoja cha Tanzania walikamatwa na kushtakiwa kwa uzuraji mwaka 2018, baada ya polisi kuwakuta wakijadili mambo ya kisiasa. Washiriki walisema kwamba mamlaka zilikuwa zikitumia sheria hizi za zamani lakini ambazo bado hazijafutwa ili kuwazuia vijana ‘kukaa vijiweni’ na uwezekano wa wao kujadili mambo ya kisiasa.

9 Shirika la Kutetea Haki za Binadamu (HRW) liisema hayo kwenye mikutano na waandishi wa habari, LHRC ilijadili tuhuma za serikali kuhusu matumizi mabaya ya madaraka wakati wa uchaguzi mkuu wa Rais mwaka 2017. Vyombo vyahabari vilivopigwa faini vilishtakiwa kwa kutangaza habari za kichochesi na kukiuka Sheria ya Utangazaji. <https://www.hrw.org/world-report/2019/country-chapters/tanzania-and-zanzibar>. mara ya mwisho ilipatikana tarehe 20 Mei 2019.

10 Spurk, C & Katunzi, A. 2019. *Yearbook on Media Quality in Tanzania 2018: Synthesised Report on Overall Results*. Media Council on Tanzania and Spurk Media Consulting Ltd.

Kwa kuwa fursa ya kujieleza kwa uhuru inafungwa, watanzania wengi wanatoa mawazo ya mitandaoni. Hata hivyo, washiriki wana sema, wananchi wanaona haja ya kutumia majina bandia. Kwa vile hofu imetanda kwenye majukwaa ya mtandaoni, washiriki walisema kwamba wana wasiwasi kwamba mtindo wa wanachi binafsi na hata mamlaka kutumia vifaa vinavyo jidhesha vyenyewe kama vile kompyuta kutoa maoni mmoja ili kuficha utambulisho wao, kwa upande mmoja, na kwa upande mwininge kuweza kupata utambulisho wa watumiaji wa mitandao.

Hata hivyo, siyo kila mmoja anahofia kusema anachotaka kwa njia tofauti ambayo inaweza kumchanganya mgeni- ambayo mshiriki mmoja alielezea kwamba inatokana na utamaduni ‘uliopo wa viwango tofauti’. Vyanzo vichache vyahabari, kama vile gazeti la *Tanzanite*, vimebakia gumzo kwa kiasi kikubwa. Kwa kuangalia kile wanachowenza kukiandika na kukikana, mtu anaweza kudhani kwamba kuna uhuru wa kujieleza Tanzania’, alisema mmoja wa washiriki. Washiriki walidai kwamba vyombo hivi vinaendeshwa na kuwezeshe na watu wanaopendelea serikali na hivyo havina madhara kwa utawala.

Kwa ufupi, sheria kandamizi za vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa zimeathiri matumizi ya haki ya uhuru wa kujieleza Tanzania kwa waandishi wa habari na wananchi halikadhalka. Hali hii imekuwa na athari hasi kwenye weledi wa waandishi wa habari na wanazuoni wengine kama vile watafiti na watetezi wa haki za binadamu kufanya kazi zao, lakini pia ubora wa uhandishi wa habari na mawasiliano mengine. Katika mazingira yaliyopo, washiriki walihisi kwamba ilikuwa vigumu kutegemea kwamba wananchi, wakiwemo waandishi wa habari, wanatumia haki zao za uhuru wa kujieleza pasi na hofu.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria			✓					✓		
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓	✓		✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria					✓				✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria										
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.0

2006: 2.1; 2008: 2.8; 2010: 2; 2012: 3.3; 2015: 2.7

1.3 HAKUNA vizingi vya kisheria kwa uhuru wa kujieleza au sheria zinazoingilia utendaji wa vyombo vya habari (mathalan, siri za kiofisi, ukosoaji na matakwa ya kisheria)

Kwa takwimu za hivi karibuni, Tanzania ilikuwa na vifungu vya sheria takriban 24 ambavyo vinaweza kutumiwa kukanyaga haki za raia za uhuru wa kujieleza na

uhuru wa vyombo nya habari. Washiriki walitoa mfano wa Sheria ya Magereza, Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Usalama wa Taifa, Sheria ya Maeneo na Sehemu Zilizozuiliwa, Sheria ya Watu Wasiokubalika na hata Sheria ya Huduma za Vyombo nya Habari kama mionganini mwa sheria kandamizi zaidi na zenye kutumiwa mara nydingi.

Sheria ya Maeneo na Sehemu Zilizozuiliwa, kama iliyio Sheria ya Watu Wasiokubalika, iko nje kabisa ya mipaka ambayo inaweza kuwa na tafsiri anuai na zinazoweza kukiukwa kwa urahisi. Sheria hii inazua matumizi ya umma ya taarifa zinazopatikana kwenye sehemu zilizoainishwa kwamba zimezuiliwa (kwa mtizamo wa waziri mwenye dhamana), bila kujali kwamba ina maslahi halali ya umma na ya kiusalama). Mmoja wa wanajopo alisema kwamba umma haukulishwa kuhusu orodha ya maeneo na sehemu ambazo zimezuiliwa, lakini bado wakiukaji wanakabiliwa na hatari ya kifungo cha miaka 20 gerezani endapo watatiwa hatiani.

Washiriki walibainisha kwamba kwa kadri itakavyokuwa na mashiko ya kisheria, serikali ina kawaida ya kufukua sheria zilizokwishakusahaulika zamani na kuzitumia. ‘Hatuzungumzii tena sheria hizi kandamizi kwa vile hatutaki kuwakumbusha uwepo wake.’

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria		✓	✓			✓	
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria				✓		✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria							
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria							

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.8

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: n/a; 2012: n/a; 2015: 1.8

1.4 Serikali inaheshimu mikataba ya kikanda na ile ya kimataifa kuhusu uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo nya habari

Tanzania ni nchi ya pande mbili – ni istilahi ya kitaalam inayotumiwa na sheria ya kimataifa kuelezea nchi ambayo inazitenga sheria zake za ndani na mikataba ya kimataifa na mikataba mingineyo. Matokeo yake, mikataba ya kimataifa inayoridhiwa na Tanzania haichukuliwi kama sheria moja kwa moja. Endapo mikataba hiyo haijapata ‘tafsiri’ ya sheria za kitaifa, haitambuliki kama sheria ndani ya Tanzania. Wanajopo walisema kwamba kwa sababu ya utaratibu huu, mikataba ya kimataifa inayohusu uhuru wa kujieleza ambaa imeridhiwa na Tanzania ni vigumu kuheshimiwa nchini.

Washiriki walieleza kwamba, pale serikali inapoona mikataba ya kimataifa inafaa kwa maslahi yake, basi vifungu nya mikataba hiyo hujumuishwa kwenye sheria

za nchi 'kidogo kidogo'. Washiriki walikuwa pia na mtazamo kwamba mamlaka zilionekana zaidi kutoitambua kabisa mikataba ya kimataifa, ambayo pia inashindwa kuiheshimu. Mathalan, Tanzania hajatimiza wajibu wake wa kutoa taarifa ya mara kwa mara kuhusu hali ya uhuru wa waandishi wa habari na haki za binadamu kwa Umoja wa Afrika na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu, ambayo inazitaka nchi wanachama kutoa taarifa kuhusu mambo hayo. Kwa kumalizia, mmoja wa washiriki alisema, 'dhamira yetu kwa viwango yya kimataifa yya haki za binadamu, hata kwenye mahakama, ni ndogo sana kiasi kwamba hata huwa hatuna tabia ya kusema hilo.'

Kumekuwepo na jitihada za kupima hali ya pande mbili za Tanzania na tabia yake ya kutoitambua mikataba ya kimataifa kwa ujumla wake. Mnamo mwaka 2019, Mahakama ya Afrika Mashariki(EACJ) ilitoa umuzi kwamba vipengele vingi vya Sheria ya Vyombo vya Habari vilikuwa kinyume na uhuru wa kujieleza na uhuru wa wanahabari kama ilivyolezwa kwenye Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mahakama ya Afrika ya Mashariki iliitaka Tanzania kufuta vipengele hivyo, hasa vile vinavyohusu uchochezi, udhalilishaji na utoaji wa taarifa za uongo. Umoja wa Uhuru wa Vyombo vya Habari uliipongeza hukumu hiyo¹¹ kama hatua muhimu katika kupigania uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari Tanzania ambao unaendelea kuzorota. Tanzania imekata rufaa dhidi ya hukumu hiyo na wakati AMB ikiendelea, vipengele kandamizi vya Sheria ya Vyombo vya Habari vilikuwa bado vinatumika.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria												
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria												
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa yya kiashiria												
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria												
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria												

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.1

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.2; 2012: 3.3; 2015: 2.5

1.5 Machapisho hayahitaji kupata kibali cha kuchapisha kutoka kwa mamlaka husika

Nchini Tanzania, ni kinyume cha sheria kuchapisha gazeti na vyanzo vingine vya habari kwa maandishi bilä kupata kwanza leseni kutoka serikalini. Hitaji hili la leseni linahusu kuuza, kusambaza, kuingiza na kutoa habari kwa maandishi popote nchini. Sheria hii inampa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari au mwakilishi wake kukataa maombi ambayo hayakidhi matakwa ya leseni na pia kufungia au kufuta leseni 'endapo mwenye leseni anashindwa kuzingatia

11 Angalia kwa mfano CPJ. Inapatikana mtandaoni kwa anuani: <https://cpj.org/2019/03/east-african-court-rules-that-tanzanias-media-serv.php>.

masharti yaliyowekwa'.¹² Masharti ya leseni ya magazeti yameelezwa kwenye Kifungu cha 7 hadi cha 16 cha Kanuni ya Huduma za Magazeti ya Mwaka 2017. Kanuni hii inaeleza kwamba leseni itaongezewa muda kila mwaka, na waombaji wanapaswa kulipa ada ya awali pamoja na ada ya mwaka ya kuongeza muda wa leseni (Kifungu cha 12 & 13).

Washiriki walisema kwamba mfumo wa utoaji leseni ultengenezwa maksudi ili kuendeleza udhibiti wa serikali dhidi ya vyombo vya habari kwa njia ya maandishi, hasa kwa kutumia mamlaka isivyo ili kukataa kutoa leseni, na kufungia au kufuta leseni. Wanajopo walikuwa na hisia kwamba sharti la kuongeza muda wa leseni kwa mwaka liliwezesha serikali kuweka kitanzi cha kudumu kwenye shingo ya vyombo vya habari vya kimaandishi na kuviveka chini ya udhibiti. 'Gazeti linapokuwa limepewaa leseni, serikali hulitupia macho, 'alisema mmoja wa washiriki. 'kama utaonekana hufai baada ya kuanza uchapishaji, inakuwa ni vigumu kuongeza muda wa leseni.'

Mamlaka zimefungia leseni za magazeti mara nyingi kwa miaka iliyopita, kwa mujibu wa washiriki, taarifa za habari na mashirika yasiyo ya kiserikali. Mifano halisi ni kama *Mawio* (ambalo lilifungiwa kwa miaka miwili mwaka 2017), na *Mseto* (ambalo lilifungiwa kwa miaka mitatu mwaka 2016). Mwaka 2018, Mahakama ya Afrika Mashariki ilipindua uamuzi uliofanywa na mamlaka kufungia leseni ya gazeti la *Mseto*, kwa madai kwamba zuio hilo lilikuwa 'halina msingi na ni kichekesho,' kulingana na makala yaliyoandikwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Utetezi wa Kisheria kwa Vyombo vya Habari.¹³ Washiriki walitabanaisha kwamba mamlaka zimedharau uamuzi huo pamoja na maamuzi mengine kadhaa ya mahakama ambayo yalizua kufungia vyombo vya habari.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓		✓	✓		✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria			✓	✓			✓		
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria					✓	✓			
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria						✓			
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria									

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.6

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 1; 2012: 1.5; 2015: 1.2

12 Sheria ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 Kifungu cha 8 na cha 9.

13 www.mediadefence.org/news/east-african-court-overturns-tanzania's-newspaper-ban.

1.6 Vyanzo vya siri vya habari vinalindwa na sheria na/au mahakama

Tanzania haina sheria mahsusini inayotoa ulinzi kwa vyombo vya habari. Sheria kandamizi kama vile [Sheria ya Mpiga Filimbi na Shaidi] hazitumiki moja kwa moja kulinda vyanzo vya siri vya habari. Hata hivyo, washiriki walisema kwamba wananchi kwa ujumla wanajua kwamba waandishi wa habari hawatakiwi kuweka bayana vyanzo vya siri vya habari kama kitu cha kawaida katika uhandishi wa habari. Kwa hivyo, kwa kuzingatia kanuni hizi zinazokubalika kwa ujumla, waandishi wa habari na taasisi za habari mara nyingi huwa wanaamua kulinda vyanzo vyao vya habari.

Pamoja na hayo, kukosekana kwa kinga ya kisheria mara nyingi husababisha bugudha kwa waandishi wa habari. Washiriki walisema kwamba ilikuwa kawaida kwa waandishi wa habari kuteswa na kubinywa kwa njia nyinginezo ili wabainishe vyanzo vyao vya habari. Mathalan, waendeshaji wa *Jamii Forums*, jukwaa la mtandaoni ambalo huwawezesha wananchi ‘kuthubutu kuongea kwa uhuru’, mara nyingi limekuwa kwenye mbinyo ili kubainisha utambulisho wa wachangiaji wanaotumia majina bandia. Kwa mtazamo wa washiriki na taarifa za habari, mwaka 2016 askari polisi waliwakamata waendeshaji wa jukwaa hilo, Maxence Melo Mubyazi na Micke Williams na kuwafungulia mashtaka kwa kuzuia haki kutendeka kwa kukataa kutoa taarifa za wanachama wao.¹⁴ Wawili hao walishaktiwa chini ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao na endapo watatiwa hatiani, watakibiliwa na adhabu ya kulipa hadi Shilingi milioni tatu za Kitanzania; sawa na Dola 1,300 za Kimarekani, kifungo cha muda usiopingua mwaka mmoja jela, au adhabu zote mbili. Waanzilishi hao wa *'Jamii Forums* wamekuwa wakienda na kurudi mahakamani kwa vile mamlaka zinalazimisha kupewa taarifa kuhusu wanachama.’

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria		✓				✓	✓			
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria										
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.3

2006: 1.6; 2008: 2.3; 2010: 1.8; 2012: 1.3; 2015: 1.2

14 Angalia kwa mfano taarifa ya habari ya BBC ya tarehe 16 Disemba 2016. Inapatikana mtandaoni kwa anuani hii://www.bbc.com/news/world-africa-38341151. Mara ya mwisho ilipatikana tarehe 22 Mei 2019.

1.7 Taarifa za umma zinapatikana kwa urahisi kwa umma na zinatambulika kisheria

Baada ya miaka minge ya ushawishi wa vyombo nya habari na watetezi wa haki za binadamu, hatimaye Tanzania ilipitisha Sheria ya Upatikanaji wa Habari ya mwaka 2016. Kifungu cha 5(1-3) cha sheria hiyo kinasema kwamba:

Kila mtu atakuwa na haki ya kupata habari ambayo iko chini ya udhibiti wa mwenye habari hizo. Mmiliki wa habari, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 na sheria nyinginezo zozote zilizo kwenye maandishi, atatoa taarifa kwa umma au, akiombwa kufanya hivyo, kwa mtu yejote, taarifa anazozimiliki yeye. Hakuna chochote katika Sheria hii ambacho kitakwamisha au vinginevyo kuzuia matakwa ya sheria nyingine yoyote ya mamlaka ya umma kutoa taarifa.

Sheria hiyo (Kifungu cha 7-9) kinabakiza kanuni za wajibu wa kutoa taarifa, wajibu wa kutunza taarifa na wajibu wa kuandika taarifa fulani. Miongoni mwa vifungu vingine, sheria inazitaka mamlaka kuteua maafisa habari kwa ajili ya ‘kushughulikia maombi ya taarifa na kutoa usaidizi kwa mtu anayetafuta taarifa hizo’. Sheria inabainisha taratibu za kupatiwa taarifa kwenye Vifungu nya 10 na 11, ambazo ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa watu wasiojua kusoma na kuandika na watu wenye ulemavu.

Pamoja na hatua hizi chanya, washiriki walisema kwamba Sheria ya Upatikanaji wa Habari bado haijitoshelezi. Mathalan, hakuna uwajibikaji kwa wamiliki wa habari ambao hawataheshimu maombi ya habari. Walifanya ulinganisho na India ambapo sheria kama hiyo inasema kwamba afisa habari atakayeshindwa kuheshimu maombi ya habari anawajibika kama yeye. Sheria ya Tanzania pia inawapa maafisa habari au watu wanaokaimu nafasi hizo, hadi mwezi mmoja ili kujibu maombi ya habari, na hivyo kuweka kigingi kwa watu ambao wanaoweza kuhitaji habari kwa haraka kama vile wanahabari na wanasheria. Aidha, Kifungu cha 18 kinaweka mipaka kuhusu namna ambayo habari zilizotolewa zinaweza kutumiwa, na kueleza muda wa kifungo cha hadi miaka miwili jela kwa mtu atakayekutwa na hatia ya kubadilisha habari zilizopatikana kwa njia ya ombi la Uhuru wa Habari (FOI).

Tangu Sheria ya Upatikanaji wa Habari ilipopitishwa, wanajopo wanasema kwamba, kwa mshangao, upatikanaji wa habari umekuwa mgumu zaidi kwa umma na kutolea mfano tafiti mbili zilizofanywa na Taasisi ya Vyombo nya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) na Baraza la Habari Tanzania, ambazo zilionesha kwamba sheria hii hajaboresha upatikanaji wa habari. Washiriki walieleza kwamba kwa utaratibu wa kuteua maafisa habari, baadhi ya mamlaka za umma – kama vile serikali za mitaa, ambazo kiasili huwasiliana na wapiga kura, wameacha utaratibu wao wa kutumia mbao za matangazo na njia nyinginezo za mawasiliano. Kumekuwepo pia na kushuka kwa haraka kwa upatikanaji wa habari kwenye tovuti za kiofisi na mitandao mingine ambayo ilikuwepo chini ya utawala wa uwazi kabla ya mwaka 2016. Badala ya kuendeleza, washiriki waliona kwamba Sheria ya Upatikanaji wa Habari ilikuwa imeweka vikwazo kwa upatikanaji wa habari.

Kuna sababu nyingi zinazofanya kuwe na mtizamo hasi. Kubwa kuliko zote inaonekana kuwa kutokujitambua mionganoni mwa wamiliki wa habari, kama vile manispaa, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs) na maafisa habari kuhusu majukumu yao. Mmoja wa washiriki alielezea hali hii kama ifuatavyo, 'Wakati mwininge, afisa habari anawenza akakuambia yeye si mzungumzaji wa Mkurugenzi Mtendaji. Pamoja na kwamba sheria inampa mamlaka afisa habari kutoa habari na kuwasaidia wale wanaotafuta habari, baadhi yao bado watakuambia kwamba wanahitaji idhini ya wakuu wao wa kazi au DED. 'Wakati huo huo, baadhi ya wilaya zimeacha utaratibu wa kutoa taarifa kwa umma kwa kutumia njia nyingine zilizokuwa zinatumia hapo kabla, kwa sababu wanahisi kwamba taarifa zote kwa sasa lazima zitolewe na maafisa habari.'

Kwa kiasi kikubwa, washiriki walliona kwamba Sheria ya Upatikanaji wa Habari ilikuwa imeirudisha nchi nyuma badala ya kuisaidia kusonga mbele. Walibainisha kwamba umma haukuwa tena na uwezo wa kupokea taarifa kwa muda muafaka kama ilivyokuwa hapo kabla wakati wilaya zilipokuwa na utaratibu wa kutumia viongozi wa mtaa ili kuwasilisha taarifa kwa wapiga kura. Kwa kuzingatia wajibu finyu wa kisheria wa kuheshimu maombi ya taarifa, mamlaka za umma zinatoa tu taarifa ambazo zinakidhi maslahi yao, ambapo maslahi haya yanakuwa hayana wigo mpana. Hata hivyo, kwa sababu za mahitaji ambatizi, baadhi ya taasisi za umma kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) mara nyingi hutoa taarifa kwa umma kwa wakati.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria				✓										✓	
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓	✓			✓			✓					✓		
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa yya kiashiria						✓	✓		✓					✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi yya kiashiria															
5	Nchi inakidhi vipengele vyote yya kiashiria															

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.2

2006: 1.1; 2008: 1.3; 2010: 1.6; 2012: 2.5; 2015: 1.6

1.8 Tovuti, blogu na majukwaa mengine ya kidijitali hayahitaji kusajiliwa na; au kupata idhini kutoka kwa mamlaka za serikali

Njia za mawasiliano mtandaoni (kwa tafsiri ya redio za mtandaoni, Luninga za mtandaoni, blogu na vyanzo vingine vya mtandaoni) zinawajibika kupata leseni ya miaka mitatu ambayo hutolewa na TCRA. Sheria za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (maudhui ya mtandaoni) ya mwaka 2018 zinaweka ada ya awali kwa huduma za mtandaoni ya shilingi za kitanzania milioni moja (sawa na Dola za Kimarekani 453, kabla ya ada ya mwaka na ada ya kuongeza muda wa leseni ya kiwango sawa na hicho. Tozo nyiningezo ni pamoja na ada ya maombi ya leseni ya shilingi za kitanzania 100,000¹⁵ (sawa na US\$43). Hata pale ambapo masharti ya kifedha yametmizwa, sheria inaipa TCRA mamlaka ya kufuta leseni ya chombo cha mtandaoni 'endapo vigezo na masharti yatakiukwa'.

Sheria hizi zinaonekana kuwa kandamizi na zenye lengo la kudhoofisha majukwaa yaliyopo ya kujieleza kwa uhuru. Zinaathiri majukwa ya mtandaoni na watumiaji wa mitando ya kijamii na, kwa maelezo ya mmoja wa washiriki, wamiliki na watumiaji wa blogu Tanzania wanaoishi nje ya nchi pia.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>									
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>									
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria										
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria										
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.1

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 3; 2012: 4.8; 2015: 4.7

15 Rasimu ya pili ya Sheria ya Mwasiliano ya Kielektroniki na Posta (mtandaoni) ya mwaka 2081, ambayo pia iliweka viwango vya ada ya leseni kwa matangazo ya redio na luninga mtandaoni.

1.9 Serikali haioneshi nia ya kuzuia au kuchuja habari za mtandaoni isipokuwa kwa matakwa ya kisheria ambayo yanaruhusu makatazo yanayohusiana na maslahi halali na ambayo ni yalazima katika jamii ya kidemokrasia na ambayo yanatumika na mahakama huru

Washiriki walieleza kwamba kwa sababu ya sifa mbaya ya mamlaka kwa kujaribu kuzuia uhuru wa habari, kulikuwa na uwezekano mkubwa kwamba serikali ingechukua hatua madhubuti ili kuzuia au kuchuja habari mtandaoni. Pamoja na kukosekana kwa ushahidi thabiti, maoni haya yanaonekana kuwa yamejikita zaidi kwenye uelewa wa wananchi kwa sababu ya sera ya serikali. Mathalan, hatua ya serikali ya kuunganisha Moduli ya Utambulisho wa Mtumiaji (SIM) wa simu za mkononi na taarifa binafsi za mmiliki wa simu ya mkononi umesababisha wasiwasili kwamba serikali ilikuwa na nia ya kufanya udukuzi mkubwa wa taarifa za raia. Mmoja wa washiriki alidai kwamba kwa msaada wa China, kikosi cha taifa cha makosa ya mtandaoni kilikuwa kimepata maarifa na uwezo mkubwa wa kuingilia tovuti na kuzuia kusambaa kwa habari lengwa katika mtandao. Kipindi cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, mawasiliano kupitia *Jamii Forums*, jukwaa la mjadala mtandaoni na jukwaa la kupuliza filimbi, ilizuiliwa kwa njia ya ajabu kwa saa 24, na kusababisha wananchi kudhani kwamba mtandao huo ulikuwa umetekwa na wataalam kutoka Ukraine au Urusi kwa niaba ya mamlaka. Pamoja na ishara hizo za wazi za kuingilia habari mitandaoni, uhusika wa moja kwa moja wa mamlaka unaonekana wa kudhaniwa zaidi kuliko wa kuthibitika.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>							
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria								<input checked="" type="checkbox"/>
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria								
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria							<input checked="" type="checkbox"/>	

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.2

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 3.3; 2012: 4.5; 2015: 3.3

1.10 Asasi ya kiraia kwa ujumla na makundi ya ushawishi wa vyombo vya habari yanafanya jithada chanya kusaka uhuru wa vyombo vya habari

Asasi za kiraia Tanzania kwa ujumla zinadhaniwa kuwa na muundo mzuri na zina nguvu. Mara nyingi, zinaungana na vyombo vya habari kwenye mambo yanayohusu uandishi wa habari kama vile upatikanaji wa habari na kuharamisha habari zinazodaiwa kuwa kashfa. Muungano wa Haki ya Habari (CORI) unajulikana sana kwa kuhamasisha taasisi zenye mlengo unaofanana kwa ajili ya kuchagiza madai ya kimkakati na kushawishi dhidi ya sheria kandamizi za vyombo vya habari. Taasisi nyiningine ambazo mara nyingi huchagiza masuala ya uhandishi wa habari ni pamoja na Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Jukwaa la Umoja wa Asasi za Kiraia Afrika Mashariki (EACSOF). Washiriki walisema kwamba mashirika yasiyo ya kiserikali yalitumia mbini anuai na kuainisha mambo kadha wa kadha, ila mara nyingi sana yanashiriki kwenye harakati zilizoratibowi.

Harakati kama hizo za NGOs nje ya vyombo vya habari hujaziliza jithada na ushawishi unaofanywa na taasisi za vyombo vya habari. Hizi pia zinaonekana kuwa hai na zenye nguvu katika kuweka msukumo kwa haki za vyombo vya habari. Taasisi zilizo mstari wa mbele ni pamoja na Jukwaa la Wahariri Tanzania, Baraza la Habari Tanzania (MCT), Taasisi ya Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Shirika la Habari za Maendeleo Tanzania (TADIO), THRDC, Umoja wa Klubo za Wanahabari Tanzania na Taasisi ya Vyombo vya Habari Afrika ya Kusini (MISA).

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria										
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria										
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria					✓			✓	✓	✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓		✓	✓	✓	

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

4.2

2006: 2.8; 2008: 2.7; 2010: 3.2; 2012: 4.1; 2015: 4.1

1.11 Sheria za vyombo vya habari zinatokana na mazungumzo mujarabu kati ya taasisi za serikali, wananchi na makundi mengine

Kwa kiasi kikubwa, mchakato wa kutunga sheria Tanzania umehodhiwa na serikali kuu na mara nyingi hukosa mchango wa kutosha wa wadau wengine

wa kisiasa na kijamii. Kwa mujibu wa washiriki, panapokuwa na majadiliano, mawazo ambayo hayaoui na mtizamo wa serikali hayazingatiwi. Katika hali ya kupindukia, serikali hutumia makundi na watu binafsi nje ya mfumo rasmi wa kisheria kushadidia msimamo wa serikali wakati wa vikao veya majadiliano- na hivyo kuzima sauti za watu wenye mawazo kinzani.

Utamaduni huu wa utungaji wa sheria unadhihirika pia kwenye sheria zinazohusu vyombo veya habari. Ili kuzua mijadala (hata ndani ya bunge), mara nyingi mamlaka hutumia nyenzo inayoitwa 'hati ya dharura', ambayo hutumiwa kuharakisha kuitisha sheria kwa kupunguza ngazi za uchambuzi ambazo mswada unatakiwa kuititia kwenye bunge. Miaka michache iliopita, sheria mbili zenyet athari za moja kwa moja kwa vyombo veya habari zimepitishwa kwa kutumia mtindo huu. Sheria hizo ni ile ya Makosa ya Mtandaoni na ile Sheria ya Takwimu.

Washiriki walitabanaisha kwamba wakati mwininge majadiliano husababisha kuweipo kwa sheria mbaya zaidi za vyombo veya habari- watetezi wa vyombo veya habari walishindwa kuzuia kutungwa kwa Sheria ya Vyombo veya Habari na inawezekana wakawa wamesaidia kuharakisha matumizi yake. Hatua dhahiri inayoonesha kutoheshimiwa kwa madai yao, ni kwamba Sheria ya Vyombo veya Habari ilitiwa sahihi kuwa sheria kamili siku moja baada ya kikao katika makundi ya watetezi wa vyombo veya habari na mamlaka husika, ambapo watetezi wa vyombo veya habari walikuwa wametoa mapingamizi dhidi ya sheria hiyo.

Ushawishi wa umma kwenye mchakato wa kutunga sheria ulizaa matunda kwenye matukio machache. Sheria ya Upatikanaji wa Habari, mathalan, ilisimamishwa kwa mwaka mmoja kutoekana na malalamiko ya wananchi. Washiriki walisema kwamba washawishi wa vyombo veya habari walifanikiwa kuondoa kifungu ambacho kinapiga marufuku kutumia taarifa zilizopatikana kuititia ombi la FOI kwa umma. Kifungu hiki kilirithiwa na kifungu kingine chenye unafuu zaidi ingawa bado kandamizi, ambacho kiliharamisha kubadili maudhui ya habari zilizopatikana kutoka kwa ombi la FOI.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria													
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu veya kiashiria	✓	✓				✓							
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa yya kiashiria			✓			✓							
4	Nchi inakidhi vipengele vingi yya kiashiria													
5	Nchi inakidhi vipengele vyote yya kiashiria													

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliopita:

2.0

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.6; 2012: 3.8; 2015: 1.7

Jumla ya alama kwenye sekta 1:

2.2



ENEO LA 2:

**Mandhari vyombo vya habari, pamoja
na vyombo vipyta vya habari, inaonesha
mtawanyiko, uhuru na uendelevu**

2.1 Vyombo vingi vya habari (vya kimaandishi, utangazaji, mtandaoni, simu za mkononi) vinapatiakana kwa umma na wananchi wanamudu gharama zake

Kitakwimu, mandhari ya vyombo vya habari Tanzania ni mchanaganyiko na hai. Mwaka 2018, ilikisiwa kwamba Tanzania Bara ilikuwa na vituo 156 vya redio, vituo 48 vya luninga na magazeti 216, wakati Zanzibar ilikuwa na vituo 25 vya redio, na vituo vya luninga 12.¹⁶ Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa upya na wanajopo, gazeti la *Tanzanite ndo ilikuwa la mwisho kusajiliwa mwaka 2015*. Vituo vya luninga vya *EFM* na *eTV* pia vilianza utangazji mwaka huo huo.

Washiriki walisema kwamba vyanzo vya habari vya kawaida vimeweza kukua kwa haraka, hasa katika kipindi cha muongo mmoja uliopita. Hata hivyo, gharama zinazidi kuongezeka na hivyo kupunguza upatikanaji hasa kwa watu maskini waishio vijijini. Mathalan, mabadiliko katika teknolojia ya utangazaji kwa luninga kwa sasa yanailazimu familia ama kununua luninga ya kisasa zaidi au kununua king'amuji ili kuweza kufaidi channeli za bure. Kwa bei ya shilingi 1000/= za kitanzania (chini ya nusu ya Dola ya Kimarekani), bei ya gazeti inalingana na ile ya mkate. Kwa mtazamo wa washiriki, inapofikia kuchagua, watu wengi watachagua kununua mkate.

Teknolojia ya kidijitali ilipanua wigo wa vyanzo vya habari. Habari kwa njia ya mitandao zimekua kwa kasi zaidi na zinapatiakana kwa uraisi zaidi. Pamoja na huduma hizo za kidijitali, magazeti yaliyo mengi, vituo vya redio na luninga vilivyo vingi vinapatiakana mtandaoni, na hutumia mitandao ya kijamii kuwafikia watu wengi zaidi. *M-Papers*, ambao ni mfumo wa habari kidijitali, huwawezesha wananchi kujunga na huduma za magazeti na majarida kielektroniki. Utafiti wa mandhari ya vyombo vya habari ulihitimisha kwamba 'Tanzania ilikuwa ikishuhudia mabadiliko ya kimtazamo kwenye anga la kimtandao'.¹⁷

Taarifa hiyo iliangazia kwamba:

Katika kipindi chamiakasitailiyopita, matumizi ya mtandao yameongezeka kutoka asilimia 17 mwaka 2012 na kufikia asilima 45 mwaka 2017. Hadi mwezi Septemba 2018, watanzania wapatao 22,995,109 walikuwa na huduma ya mtandao, huku wengi wao (19,006,223) wakitumia mtandao kuititia simu zao za mkononi. Mabadiliko haya, ingawa yanatokea zaidi mijini, yana mchango chanya kwenye upatikanaji wa vyombo vya habari kwa wananchi kwa vile raia wanaweza kufikia vyombo vya habari kuititia mitandao kadha wa kadha ya kijamii. Kwa kuongezea, hali hii inatoa fursa kwa raia kutoa maoni yao kwenye mijadala mbalimbali na ukuaji wa upashaji habari wa kiraia mtandaoni (Spurk&Katunzi, 2018).

Upatikanaji wa habari kwa njia ya mtandao unaathiriwa tu na gharama za kupata huduma hiyo. Ingawa watumiaji huhitaji chini ya nusu ya Dola ya Kimarekani

¹⁶ Ibid.

¹⁷ Ibid.

kupata gigabaiti moja ya data, washiriki walisema kwamba gharama hiyo ilikuwa bado juu kwa wananchi walio wengi. Kwa muhtsari, Tanzania ina wigo mpana wa vyanzo vya habari, lakini upatikanaji wa vyanzo hivi mara nyingi umeathiriwa na gharama, teknolojia na miundombinu.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria																			
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria																			
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria																			
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria																			
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria																			

Wastani wa alama:

3.5

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 2.9; 2008: 2.8; 2010: 3; 2012: 3.3; 2015: 3.6

2.2 Upatikanaji wa vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi kwa wananchi hauzuiliwi na mamlaka za serikali

Upatikanaji wa vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi uko wazi na hauna vizingiti Tanzania. Washiriki walisema kulikuwa na wigo mpana wa magazeti ya nje katika mzunguko na wananchi wanaweza kupata matangazo ya nje kuititia satelaiti na mkongo.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria																			
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria																			
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria																			
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria																			
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria																			

Wastani wa alama:

4.8

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 3.1; 2008: 4.1; 2010: 3.8; 2012: 4.3; 2015: 4.7

2.3 Uhuru wa wahariri wa magazeti na vyanzo vya habari mitandaoni zinazochapishwa na mamlaka za umma unalindwa vya kutosha dhidi ya kuingiliwa kisiasa kusiko kwa lazima

Tanzania ina magazeti mawili yanayomilikiwa na serikali, ambayo ni *Daily News na Habari Leo*. *Magazeti haya mawili na matoleo yake ya matandaoni kwa kiasi kikubwa yanaonekana kama kipaza sauti cha serikali iliyoko madarakani na sehemu ya nyenzo ya dola*. *Matokeo yake ni kwamba havina uhuru wa uhariri*.

Washiriki waliezea utamaduni wa kuegemea upande mmoja, uchujaji habari/kujichuja na uhandishi wa ‘mapambazuko’ kwenye magazeti yanayomilikiwa na serikali. Pamoja na mambo mengine, wahariri na waandishi wa habari wa *Daily News na Habari Leo* wana utaratibu wa kuzima habari ambazo siyo rafiki kwa serikali na kunyamazisha sauti za watu wenye mawazo kinzani. Uchambuzi wa maudhui kwenye gazeti la *Daily News* mwaka 2018 ulionesha kwamba gazeti hilo halikuandika habari yoyote ya kuikosoa serikali kwa mwaka mzima. Mmoja wa wanajopo alisema kwamba, ‘Unapokubali ajira *Daily News*, unajua moja kwa moja kwamba kuna habari ambazo huwezi kugusa.’

Ingawa washiriki walikubaliana kwamba magazeti yanayomilikiwa na serikali hayana uhuru wa uhariri, baadhi yao walidhani kwamba kukosekana kwa uhuru kunaweza kusiwe na tatizo. Mmoja wa washiriki alisema kwa hisia kwamba kama sehemu ya chombo cha serikali, magazeti yanayomilikiwa na serikali yanapaswa kuangaliwa kama vyombo vilivyo kwenye mikono ya mamlaka ili kuchagiza utendaji wa serikali.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria			✓	✓	✓			✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓	✓		✓			✓		
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria						✓	✓		
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria									✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria									

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.9

2006: 2.4; 2008: 1.8; 2010: 1.9; 2012: 2.3; 2015: 1.8

2.4 Uwazi wa umiliki wa vyombo vya habari unatolewa na kulindwa na sheria

Umliliki wa vyombo vya habari Tanzania unathibitika kiraishi kwa vile mamlaka yana orodha ya wamiliki wa makampuni na wadau chini ya Sheria ya Makampuni. Hata hivyo, washiriki walisema kwamba daftari la umiliki wa makampuni linaweza lisioneshe wamiliki halisi wa vyombo vya habari. ‘Watu wanaweza kuunda

makampuni na makampuni kuunda makampuni mengine kiasi kwamba kujua ni nani hasa yuko nyuma ya chombo cha habari, ni lazima ufanye uchunguzi wa kina,' alisema mmoja wa washiriki. Mshiriki mwingeine aliongezea kwamba inawezekana kwamba mmiliki halisi wa vyombo nya habari akawatumia watu wengine na makampuni kama watangulizi.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria													
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria	✓	✓		✓							✓	✓	
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria		✓	✓								✓	✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria				✓	✓	✓	✓						
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria													

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.8

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: n/a; 2012: n/a; 2015: 3.8

2.5 Sheria zinajitosheleza kuendeleza ushindani na kuzuia msongamano na kuhodhi vyombo nya habari

Sheria ya Ushindani Huru ya mwaka 2003 inapaswa kuzuia mrundikanao na kuhodhi katika sekta mbalimbali, ikiwemo sekta ya habari. Hata hivyo, kuitendaji, mrundikano wa vyombo nya habari ni mkubwa Tanzania. Utatifi uliofanywa mwaka 2018¹⁸ na MCT na Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka ulionesha kwamba vyombo nya habari Tanzania vilikuwa vimeodhiwa na watu wachache sana.

Utatifi huo ulibainisha kwamba:

Baadhi ya makundi makubwa ya vyombo nya habari yanamilikiwa na wamiliki ambao hudhibiti makampuni yenyen wigo mpana wa maslahi kwenye sekta nyingine za biashara. Mathalan, marehemu Dr. Reginald Mengi, ambaye ni mwanzilishi wa IPP Media Group, alikuwa amejikita kwenye biashara ya vinywaji nya chupa, kwenye bidhaa za nyumbani na bidhaa za urembo na uchimbaji madini. Vile vile alikuwa na nia ya kuwekeza kwenye uchimbaji wa mafuta na gesi, viwanda nya magari na madawa. Mfano mwingeine ni ule wa Said Salim Bakhresa, bilionea aliyejiendeza mwenyewe na aliyeanzisha Azam TV, ambayo inalipiwa Afrika ya Mashariki nzima. Kundi lake la Bakhresa Group kwa leo ni miongoni mwa taasisi kubwa zaidi Afrika ya Mashariki, ikijumuisha biashara ya vyakula na vinywaji, ufungashaji, huduma za usafiri wa majini na biashara ya mafuta ya magari. Kuna hatari ya wamiliki wa vyombo nya habari wenye maslahi anuai ya kibiashara kutumia vyombo vyao vya

18 Angalia 'Nani Anamiliki Vyombo nya Habari Tanzania?' Inapatikana mtandaoni kwa anuani hii: <https://rsf.org/en/reports/who-owns-media-tanzania>. Mara ya mwisho ilipatikana tarehe 29 Mei 2019.

habari kwa lengo la kukuza na kuwezesha kampuni zao weneyewe – na hivyo kusahau maudhui yenye maslahi mapana ya kijamii.

Washiriki walisema kwamba eneo mojawapo la tatizo hilo ni kushindwa kwa Sheria ya Vyombo vya Habari kushughulikia tatizo la msongamano wa vyombo vya habari. Washawishi wa vyombo vya habari wameshindwa kwa miaka mingi kushawishi mamlaka kubadilisha sheria inayomruhusu mmiliki mmoja kumiliki vyombo anuai vya habari. Matokeo yake, tasnia ya habari inadhibitiwa na watu wasiofikia hata watano pamoja na washirika wao.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria	✓		✓	✓	✓	✓	✓		✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria		✓								
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.6

2006: 1.6; 2008: 2.4; 2010: 1.7; 2012: 2.7; 2015: 2.8

2.6 Serikali inakuza wigo mpana wa mandhari ya vyombo vya habari yenye vyanzo endelevu kiuchumi na huru

Tanzania ina wigo mpana ya vyombo vya habari ambapo vyanzo anuai vinatoa huduma ya habari kwa makundi anuai. Hata hivyo, washiriki walisema kwamba hayo si matokeo ya sera ya serikali. Kinyume chake, hazina ya sheria za kufisha imetumiwa kuhujumu mazingira ya kuwepo kwa vyombo vya habari endelevu kiuchumi na huru. Ada za leseni kwa vyombo vyote vya habari, mathalan, ni kubwa na zinakatisha tamaa. Mali ghafi zinazotumiwa na vyombo vya habari hazina msamaha wa kodi na hata radio za kijamii lazima zilipe ada kubwa ya leseni kila mwaka.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓	✓	✓	✓			✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria							✓	✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓									
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.5

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 1.8 ; 2012: 1.3; 2015: 2.8

2.7 Vyombo vyote vinazingatia usawa kwa jinsia zote

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa miaka mingi, wanaume bado wanamatamaki kwenye taarifa za habari. Washiriki walisema kwamba maisha ya kijamii na kiutamaduni ambayo yanawafanya wanawake waonekane kama kivuli kwenye jamii kwa kiasi fulani yanababisha uchache wa wanawake kwenye vyombo vya habari. ‘ni wachache kati yao wako radhi kuongea, hata wanapoombwa kufanya mahojiano.’

Uwakilishi wa wanawake kwenye vyombo vya habari pia unaakisi jamii ambayo kwa kiasi kikubwa imekaa kimfumo dume. Kwa ujumla, wanaume wanatawala anga la umma na kudhibiti habari na mada za kijamii na wigo wa habari. Habari zinazohusu wanawake zinapopenya kwenye vyombo vya habari, zinawasilishwa kuititia lensi ya wanaume na huwa zenye msisimuko na kudhalilisha.

Washiriki walieleza kwamba vyombo vya habari pia huwa na tabia ya kuwabagua wanawake kwa kificho. Wakati wa kampeni za kisiasa, mathalan, wagombea wa kiume huwa wanapata muda mwingu zaidi kuliko wenzao wa kike. ‘Kuna wanawake wachache wenye nguvu ambaeo wako radhi kuongea lakini ambaeo hawapatiwi fursa,’ alisema mmoja wa washiriki.

Vyombo vya habari vimeshindwa kukosoa imani potofu dhidi ya wanawake na badala yake vimeshiriki kuziendelea imani hizo:

Rais alipowakataza wasichana wenye ujauzito kuendelea na masomo, vyombo vya habari viliikimbia habari hiyo bila kuhoji utata katika sera hiyo. Wanapotoa habari zinazohusu wanawake, wanaonekana kama wahanga. Habari zinakuwa za udhalilishaji na zenye imani potofu.

Vyombo vichache vya habari vimefanya mabadiliko ya makusudi ya sera ili kuongeza sauti za wanawake. Mathalan, waandishi wa habari wa ndani na watangazaji wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) wanatakiwa kujumuisha wanawake kwenye taarifa zao na vipindi vyao. Redio za kijamii pia zimefanya mabadiliko kwa miaka mingi ili kuongeza sauti za wanawake na mada zenye maslahi kwa wanawake.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria		✓										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓		✓		✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria			✓					✓				
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria												
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria												

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.1

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.7; 2012: 3.4; 2015: 2.6

2.8 Vyombo vyote vya habari vinawakilisha mchanganyiko wa wanajamii kwa haki

Tanzania ni jamii mchanganyiko ambayo ina makabila na lugha za kijamii zaidi ya 120. Hata hivyo, mchanganyiko huu hauakisiwi kwenye vyombo vya habari kwa kuwa sheria inazuia matangazo kwa lugha za kijamii. Kuruhusu matangazo kwa ‘Kiingereza fasaha na Kiswahili pekee’ ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kudumisha umoja wa kitaifa na kuzuia uwezekanao wa makabila machache kuwa na nguvu kuliko mengine. Hata hivyo, washiriki walikosoa njia hiyo kama isio na ushahidi. ‘Hii inamkosesha mtanzania wa kawaida sauti kwenye vyombo vya habari.’ ‘Sisi ni nchi yenye mchanganyiko lakini bado tuko mbali katika kuukubali mchanganyiko na wingi wetu.’ Washiriki walisema pamoja na lugha, kulikuwa na matatizo kuhusu namna ambavyo makundi mbalimbali ya kijamii (hasa wale wachache) yanawakilishwa kwenye vyombo vya habari: kwa ujumla vyombo vya habari hutengeneza imani potofu kuhusu Waarabu na Wahindi wa Tanzania. Aidha, ni vipindi vichache sana huwalenga watu wenye ulemavu. Matumizi ya lugha ya alama kwenye luninga ni nadra na hakuna magazeti yanayotumia nukta nundu.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		<input checked="" type="checkbox"/>		<input checked="" type="checkbox"/>							
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>		<input checked="" type="checkbox"/>				<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>			
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria											
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria											

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.2

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.6 ; 2012: 2.8; 2015: 3

2.9 Vyombo vya habari vinagusa maeneo yote ya kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa, mitazamo ya kitaifa na kimaeneo, ikiwa ni pamoja na kwa njia ya taarifa za kiuchunguzi

Tanzania itafanya uchaguzi mwaka 2020. Wakati wa AMB hii (takriban mwaka mmoja kabla ya upigaji kura) washiriki walisema kwamba kulikuwa na habari chache sana kuhusu uchaguzi huo. Walieleza kwamba ufinyu wa habari kuhusu uchaguzi unaokaribia unaonesha kupungua kwa kasi kwa habari za kisiasa kwa ujumla. Kutokana na athari za kuogofya za fursa za kisiasa zinazozidi kudorora, waandishi wa habari wamegeukia kwenye mada ambazo zinadhaniwa kuwa na hisia kidogo kama vile maslahi ya kibinadamu, utamaduni na shughuli za serikali. Uhandishi wa habari za kiuchunguzi pia umeathirika, na ni miradi

michache tu iliyochunguzwa kila mwaka. Pamoja na hivyo, taarifa za habari kwa ujumla zimejikita maeneo ya mijini. Ni kampuni chache tu zenye waandishi wa habari kwenye maeneo ya pembezoni mwa nchi. Washiriki walieleza kwamba jamii za vijijini zinapewa nafasi wakati wa ziara za viongozi wakuu wa serikali kama vile ziara za mawaziri.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria								
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓	✓	✓	✓		✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria	✓		✓		✓	✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria								
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria								

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.6

2006: 3.1; 2008: 2.3; 2010: 3.2; 2012: 3.3; 2015: 3.9

2.10 Watangazaji binafsi wanatoa vipindi vyenye viwango vinavyotakiwa vya maslahi ya umma

Watangazaji binafsi wanatakiwa na sheria ‘kukuza uwelewa wa wananchi kuhusu masuala mbalimbali yenye maslahi ya kitaifa’ na ‘kutangaza na kuandika habari au masuala yenye umuhimu kitaifa kama itakavyo elekezwa na serikali.’¹⁹ Washiriki walisema watangazaji binafsi wanajitahidi kuzingatia matakwa haya lakini pia wanabanwa na hitaji la kuwafikia watu wengi ili kutengeneza vipindi vyenye maslahi kwa umma. Hata hivyo, inaonekana kuwepo na kutolewana kati ya watangazaji na serikali kuhusu maana ya maslahi ya umma. Mathalan, washiriki walieleza kwamba watangazaji walitozwa faini kwa kutoa taarifa kuhusu madai ya kuwepo dosari wakati wa uchaguzi mdogo wa madiwani tarehe 26 Novemba 2017.²⁰

19 Sheria ya Vyombo vya Habari Tanzania, Kifungu cha 7.2.

20 Mamala ya Mawasiliano Tanzania yalivitoza faini vituo vitano vya luninga jumla ya TZS 60 milioni (\$27,000) kwa utangazaji ‘usiozingatia sheria na maadili’. Vituo hivyo vilirusha hewani tathmini iliyofanyanya na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuhusu uchaguzi mdogo wa madiwani tarehe 26 Novemba, 2017, ambapo serikali iliona haukizingatia sheria wala maadili. Ilipatikana kwa anuanī hii: <https://www.africanews.com/2018/01/03/tanzania-fines-tv-stations-for-airing-human-rights-report/>

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria						✓			✓	
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria	✓	✓		✓				✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria		✓	✓		✓	✓				
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

3.2

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: n/a ; 2012: n/a; 2015: 3.1

2.11 Nchi ina sera murua na kamilifu ya TEHAMA na/ au serikali inakuza na kutekeleza hatua ambazo zinakidhi mahitaji ya mawasiliano kwa umma, ikiwemo jamii za pembezoni

Tanzania ni kinara katika kubuni na kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ukanda wa Afrika ya Mashariki. Washiriki walisema kwamba Tanzania ni mionganini mwa nchi za mwanzo duniani kuunda teknolojia ya pochi jongefu na ina utaalam wa hali ya juu wa tiba ya masafa. Kwa kutumia mpango wa upatikanaji wa habari kwa wote, serikali hugharamia miradi ya kuunganisha maabaraa za kompyuta mashulenii na mafunzo kwa vijana. Washiriki walieleza kwamba serikali ilikuwa ikibuni njia za kusaidia mfumo wa teknolojia na wajasiriamali chipukizi kwenye teknolojia kwa kutoa fedha na mfumo mahsusii wa kodi kwa ajili ya kuwezesha mpango huo. Ushiriki wa serikali kwenye TEHAMA umeleta matokeo chanya kwenye sekta mbalimbali; hasa benki, biashara ya rejereja na biashara mtandao.

Sera mpya ya TEHAMA ilichapishwa mwaka 2016 kwa lengo la ‘kubadlisha Tanzania kuwa na uchumi unaowezeshwa na TEHAMA, na ujuzi kupitia ubunifu na matumizi endelevu ya TEHAMA ili kumnuifaisha kila mwananchi na biashara’.²¹ Washiriki walisema sera hiyo ilikuwa ya kimapinduzi na ilionesha utashi wa kisiaza wa kujenga jamii yenye ujuzi.

21 Sheria ya Taifa ya TEHAMA, 2016.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria										
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria					✓			✓		
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria		✓	✓	✓		✓	✓	✓		✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria	✓	✓	✓	✓						✓

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

4.1

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 3.6 ; 2012: 3.3; 2015: 3.5

2.12 Serikali haitumii nguvu yake dhidi ya urushaji wa matangazo ya biashara kama njia ya kuzuia maudhui ya kiuhariri

Kwa maelezo ya washiriki, serikali inatumia mamlaka yake kuhusu urushaji wa matangazo ili kuzuia maudhui ya kiuhariri. Sheria ya Vyombo vya Habari inamweka Mkurugenzi wa Idara ya Habari (DIS) kuwa msimamizi wa matangazo ya serikali. Washiriki walisema kwamba hali hii husababisha mgongano wa kimaslahi kwa vile DIS pia anawajibika kuratibu taarifa za serikali, kufanya mikutano na waandishi wa habari kwa niaba ya serikali na kufungia magazeti. Washiriki walisema haina shaka kwamba matangazo ya serikali yanaenda zaidi kwenye vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali na kwa kiasi kidogo sana kwa vyombo vinavyoikosoa serikali- kama vile magazeti yaliyo na mrengo wa upinzani. Baada ya kuona msimamo wa serikali, washiriki walisema wenye matangazo binafsi wamesita kupeleka matangazo kwenye vyanzo vya habari makini.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:²²

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓			✓		✓			
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria			✓							✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria				✓					✓	
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria	✓	✓	✓							

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

3.0

2006: 2.4; 2008: 2; 2010: 2.1; 2012: 2.2; 2015: 1.6

22 Tofauti katika alama inaweza kuwa imetokana na uelewa dhaifu wa kiashiria na jinsi ya kuamua alama. Mjadala ulionesha kwamba kwa ujumla Tanzania haikufanya vema katika kiashiria hiki.

2.13 Ukubwa wa soko la utangazaji unawezesha uwepo wa mchanganyiko wa vyanzo vya habari

Makampuni ya habari yanalalamika kwamba hawapati matangazo ya biashara ya kutosha ili kuwezesha uendeshaji. Washiriki waliona kwamba, hakika, soko la matangazo ya biashara limedorora kwa miaka mingi na kubakia na watangazaji biashara wachache tu; hasa mashirika ya mawasiliano ya simu, viwanda vya bia na mabenki. Kwenye mijadala, ilionekana kwamba sababu kuu mbili zimebadilisha sura ya soko la matangazo ya biashara Tanzania. Mosi, serikali inadhibiti sehemu kubwa ya matumizi kwenye matangazo ambayo yanarushwa kwa kuvipendelea vyombo vinavyomilikiwa na serikali na vile vya binafsi vyenye kuelemea upande wa serikali. Pili, watoaji wakubwa wa matangazo ya biashara wa zamani sasa wanamiliki vyombo vyao wenyewe vya habari. Hali hii si tu kwamba imebana soko la matangazo ya biashara, lakini pia imeondoa usawa kwenye mgao wa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara kwenye tasnia nzima.

Mmoja wa washiriki alisema vyombo vya habari pia havikuwa na uwezo wa kuvutia matangazo, akieleza kwamba:

Biashara mpya zinaanzishwa kila siku na zinahitaji kutangazwa. Tatizo ni kwamba vyombo vya habari vinawakimbilia watoaji matangazo wale wale. Kama wanatarajia kupata matangazo kutoka serikalini tu na kwenye makampuni machache, basi wanaweza wasipate ya kutosha. Redio za kijamii wanalijua hili na ndo maana wanaenda kwenye sekta isyo rasmi. Tunatakiwa tuelewe kwamba mambo ni magumu na kuacha kubagua.

Ushindani kutoka kwa majukwaa mbadala kama vile mitandao ya kijamii pia umeongezeka. Watu wengi na wafanyabiashara wadogo wameugezia matangazo ya biashara kwenye mtandao. 'Changamoto kwa vyombo vya habari ni kwenda na mabadiliko haya.'

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria																				
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓															✓		
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria				✓				✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓				✓		
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓				✓															✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria																				

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

3.0

2006: 2.1; 2008: 1.9; 2010: 2; 2012: 2.5; 2015: 2.2

Jumla ya alama kwenye sekta 2:

2.7



ENEO LA 3:

**Sheria ya matangazo ni wazi na huru;
vyombo vya umma vimebadilishwa na
kuwa vyombo halisi vya umma**

3.1 Sheria ya utangazaji inapitishwa na kutekelezwa, na inatoa mazingira mazuri kwa matangazo ya umma, biashara na jamii

Washiriki walisema sheria za utangazaji, hasa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta na Sheria ya Vyombo vya Habari zilikuwa zinabana sana. Walitolea mfano masharti magumu ya utoaji leseni, ambayo ni pamoja na ada ya mwaka ya kuongeza muda wa leseni na msururu wa faini, kama vikwazo dhidi ya ukuaji wa utangazaji kwa watu binafsi na jamii. Pamoja na sifa ya radio za jamii ya kutotengeneza faida na kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya jamii, radio hizo hazipati upendeleo wowote maalum au msamaha wa kodi.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria								
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓					
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria				✓	✓	✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓	✓					✓	✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria							✓	✓

Wastani wa alama:

3.3

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 2.6; 2008: 2.8; 2010: 2.1; 2012: 3.8; 2015: 3.3

3.2 Utangazaji unadhibitiwa na chombo huru ambacho kimelindwa ipasavyo dhidi ya kuingiliwa na sheria, na ambacho bodi yake inateuliwa kwa uwazi na kushirikisha asasi za kiraia na ambayo haihodhiwi na chama chochote cha siasa

Utangazaji unadhibitiwa na TCRA. Mamlaka haya yaliyoanzishwa kwa sheria ya bunge mwaka 2003, yanajinasibu kama 'chombo chenye uhuru-kifani'. Bodи yake inateuliwa na Rais na waziri mwenye dhamana ya sekta hiyo, kwa kuititia mchakato wa uteuzi unaongozwa na katibu mkuu wa wizara husika. Kamati ya uteuzi inajumuisha wawakilishi wawili wa sekta binafsi lakini haina maamuzi ya mwisho kuhusu wajumbe wake. Washiriki walisema TCRA haiko huru, pamoja na kwamba wajumbe wa bodi wanawakilisha wigo mpana wa utaalam. Inawajibika kwa serikali na kuangalia maslahi ya serikali.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓	✓						✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria				✓	✓	✓			
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria	✓					✓	✓	✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria						✓	✓	✓	✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria									✓

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.2

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 1.1; 2012: 3.1; 2015: 2.6

3.3 Chombo kinachodhibiti utangazaji na utoaji leseni kinafanya hivyo kwa maslahi ya umma na kuhakikisha haki na mchanganyiko wa mawazo mapana yanayowakilisha jamii kwa ujumla

Nje na udhibiti, TCRA ina wajibu wa kutoa leseni za utangazaji na kupanga na kusimamia mawanda ya matangazo ya redio. Leseni ya utangazaji inajumuisha kibali cha kujenga ‘sehemu ya kurushia matangazo, studio, multiplex headends, uplink earth stations na miundo mbinu yoyote ya kituo cha redio kama itakavyo ekeze wa na mamlaka husika’ na kuthibitisha miundombinu ya utangazaji (Kifungu cha 7 (1-2)). Washiriki walisema TCRA ‘inajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kutoa leseni’ ingawa mchakato unakuwa mrefu sana. Kwa mara ya mwisho, leseni zilitolewa mwaka 2015.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria									
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria				✓					
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria					✓	✓	✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓	✓	✓		✓	✓	✓	✓	✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria									

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

3.3

2006: 3; 2008: 2.8; 2010: 3.4; 2012: 3.5; 2015: 3.2

3.4 Vyombo vyatukio na ambayo imeteuliwa kwa njia iliyo huru na wazi.

TBC ilianzishwa mwaka 2007 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2018. Inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu na kusimamiwa na bodi ya wakurugenzi. Mkurugenzi mkuu pamoja na mwenyekiti wa bodi wanateuliwa na Rais, wakati wajumbe wengine wa bodi wanateuliwa na waziri, kila baada ya kipindi cha miaka mitatu. Wajumbe wa bodi hawana uhakika wa kumaliza kipindi chao kwa kuwa mamlaka ya uteuzi inaweza kutengua uteuzi wao kabla ya kumaliza muda wao.

Washiriki walikuwa na maoni kwamba kwa kuangalia utaratibu wa uteuzi, bodi ya TBC isingeweza kudhaniwa kuwa huru. Bodii iliopo iliteuliwa mwaka 2016²³ Pamoja na tathmini hasi ya uhuru wake, washiriki hawawafahamu wengi wa wajumbe wa bodi ya sasa na kwa hivyo wasingeweza kusema kama waliwakilisha jamii kwa ujumla.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria	✓	✓	✓	✓			✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria						✓		
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria								
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria								

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliopita:

1.6

2006: 1.5; 2008: 1.7; 2010: 1.9; 2012: 2.3; 2015: 2.1

3.5 Uhuru wa uhariri wa chombo cha umma/serikali dhidi ya ushawishi wa kisiasa unalindwa na sheria na unatumika kuhakikisha kwamba habari zinakuwa za haki na zenye uwiano na zenye kuakisi masuala yaliyopo

Sheria iliyounda TBC inaeleza kwamba ‘itahimiza mtizamo wa kitanzania kwa kuwa na wigo mpana wa vipindi’. Katika Sehemu ya 7 (1-2), sheria ya TBC

²³ Angalia taarifa mpya kupitia <https://www.thecitizen.co.tz/News/Magufuli-appoints-new-TBC-board-chairman/1840340-3086330-rtfhwg/index.html>.

inakipa chombo hiki wajibu wa kuutangazia umma na uhuru wa uhariri. Inaeleza kwamba:

Kwa kuzingatia vipengele vya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kutakuwa na Mkataba kati ya Shirika la Utangazaji Tanzania na Wazir ili kuliwezesha Shirika la Utangazaji Tanzania kuwa chombo cha utangazaji cha umma chenye wajibu wa kuhudumia watu wote.

Mkataba huo utahakikisha kuwa Shirika la Utangazaji Tanzania linatekeleza malengo yake na kutumia mamlaka yake, linakuwa na uhuru wa kujieleza, uhandishi wenyewe ubunifu na vipindi bila kuingiliwa na serikali na wadau wengine.

Washiriki walikuwa na maoni kwamba kiutendaji, TBC haikuwa na uhuru wa kiuhariri na kwa ujumla ilionekana kutumikia maslahi ya serikali iliyopo madarakani. Vilevile TBC inaonekana kama msemaji wa chama tawala na mara nyingi hudhahirisha hujuma zisizochujwa dhidi ya upinzani na sauti zenye ukinzani. Mmoja wa washiriki alisema kwamba watendaji na waandishi wa habari halikadhalika wanalazimika ‘kuufyata’ mara wanapoajiriwa TBC na kutekeleza sera za serikali, hata kama walikuwa wanahabari makini kabla ya kuteuliwa kushika nafasi walizo nazo.

Washiriki walisema kwamba watendaji waliopita ambao walijaribu kuigeuza TBC ili kuendana na uhuru wa uhariri na kuruhusu mawazo mchanganyiko wamejikuta kwenye matatizo.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria				✓			✓		✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria								✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria									
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria									

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.4

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: n/a; 2012: n/a; 2015: 2.2

3.6 Chombo cha umma kinapewa fedha za kutosha kiasi cha kukilinda dhidi ya ushawishi wa kisiasa kupitia bajeti yake na dhidi ya ulazima wa kufanya biashara

Kulingana na washiriki, TBC haikuwa inapewa fedha za kutosha na gawio la bajeti yake kwa mwaka kutoka wizarani linakidhi tu kulipa mishahara na mahitaji ya msingi ya uendeshaji- na hii inaathiri maendeleo kibiashara na mpangilio wa vipindi. Ili kuwafikia watu wengi, shirika limelazimika kuingia mkataba na radio

za kijamii ili kurusha vipindi nya TBC kama vile taarifa ya habari kwenye maeneo ya vijijini. Kwa vile luninga yake haitozwi ada, shirika linategemea sana mapato yatokanayo na matangazo ya biashara. Hata hivyo, washiriki waliona kwamba shinikizo la kufanya biashara lilikuwa na athari kidogo zaidi kwa TBC kuliko kuingiliwa kisiasa.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria			✓			✓		✓		
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria				✓						
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.8

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.1; 2012: 2.5; 2015: 1.5

3.7 Chombo cha serikali kinatoa mchanganyiko wa vipindi na aina mchanganyiko ili kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbabali, ikiwamo maudhui ya kimaeneo na vipindi vyenye ubora na kuwakilisha maslahi ya umma

TBC inatoa wigo mpana wa vipindi vinavyohusu mada anuai kuanzia siasa hadi mitindo. Hata hivyo, washiriki walisema kwamba vipindi vingi vinalenga kuelezea utendaji wa serikali na kuelemea upande chanya wa mamlaka badala ya kuangalia maslahi ya makundi yote. Ni kawaida kuona vipindi vinavyojadili mambo muhimu ya kisiasa kuondoka hewani ghafla.

Mkutano wa hadhara wa kujadili rasimu ya katiba mpya, ikiwemo matangazo mbashara ya mijadala, uliondoka hewani ghafla baada ya dakika chache tu. Baadaye ulibadilishwa na maonesho ya mapishi. Na imekuwa kawaida kwa TBC kuwa hewani na vipindl ambavyo havina maslahi halisi kuliko kuwa na vipindi nya siasa ambavyo vinatoa maoni ambayo yanatofautiana na yale ya serikali.

Baadhi ya washiriki walidai kwamba sauti kadhaa kinzani (hasa wanasiwa wa upinzani na watetezi wa haki za binadamu) wamezuliwa kuonekana TBC. Chombo hiki pia chenyewe kimelazimika kuzua vipindi vyenye wapenzi wengi hasa wanapoona kwamba hawawezi kudhibiti kile wanachoweza kukisema wazungumzaji waalikwa.

Mshiriki mmoja alielezea jinsi ambavyo kipande maarufu kilitoweka kwenye taarifa ya habari:

TBC ilikuwa na kipande cha makala kilichokuwa kinaitwa *In Between the News*, ambapo mtaalam au mchambuzi alikuwa anaalikwa kutoa maoni kuhusu matukio muhimu kwenye taarifa ya habari. Muda fulani, Rais aliwasamehe watu ambaao walikuwa wametumia fedha za umma vibaya. Kabla ya kuwa hewani, aliambiwa, "Leo inabidi uongee vizuri kuhusu serikali na kuipongeza serikali kwa kufanya kitu kizuri". Lakini alipokuwa hewani, alisema ilikuwa ni makosa kwa msamaha wa Rais kutolewa kabla ya wahusika kushtakiwa mahakamani ili kuwatia hatiani au kuwaachia huru. Kuanzia siku hiyo, kipindi cha *In Between the News* kilifutwa.

Ili kuendelea kuwa hewani, TBC ina msururu wa matangazo ya tamthiliya, orodha ya miziki na vipindi vinavyoelezea 'namna ya kuwa mzalendo na raia mwema au kuwa mke mzuri'.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria										
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria		✓							✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓									
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.4

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: n/a; 2012: n/a; 2015: 2.6

Jumla ya alama kwenye sekta 3:

2.0



ENEO LA 4:

Vyombo vya habari vina viwango vya juu
vya weledi

4.1 Viwango vya utoaji habari vinafuata kanuni za msingi za usahihi na haki

Majadiliano yalidhihirisha mgawanyiko mkubwa mionganoni mwa washiriki kuhusu viwango vya utoaji habari katika vyombo vya habari vya Tanzania kwa kuzingatia haki na usahihi.

Baadhi ya washiriki walikuwa na mtizamo kwamba utoaji wa habari na uchambuzi kwa ujumla haukuwa wa haki. Matatizo ni pamoja na uwasilishaji hafifu wa mawazo ya nyanzo vya habari na kuelemea upande wa chama fulani cha siasa au makundi ya kijamii. Kwa kiasi kikubwa, taarifa za habari na uchambuzi huwa na tabia ya kufuata mada kuu ya kisiasa na kijamii inayotekelzeza na serikali, na kutoa nafasi finyu kwa mawazo kinzani. Vyombo vya habari, hususan, havitaakisi mawazo yanayoikosoa serikali au kutoa mbadala wa misimamo rasmi iliyoolewa. Mmoja wa washiriki alisema vyombo vya habari vilikuwa na hatia ya kuendeleza mila potofu, ambazo mara nyingi husababisha mtafaruku mionganoni mwa makabila na dini ndogo.

Kwa upande wa masuala ya kiutamaduni na kiti, kuna tabia ya waandishi wa habari kuendana na kile kinachoaminiwa na kila mtu. Wakati wa kutoa habari kuhusu dini fulani, waandishi wa habari hawaendi hatua [moja] mbele [ili kupata ukweli] na wataegemeza habari zao kwenye kile kinachoaminiwa na watu wengi zaidi.

Washiriki wengine walisema kwamba mazingira ya kijamii na kisiasa ambayo waandishi wa habari wanafanya kazi ni ya kulaumiwa kwa kuwa na upendeleo katika wigo wa habari. Walisema kwamba, vyombo vya habari vya serikali vilikuwa na nia yake ya kushadidia msimamo wa serikali na visingweza kutarajiwa kujihujumu chenyewe. Walisema kwamba nguvu ya vyombo vya habari vya serikali na nyanzo vingine vya habari ambavyo viko upande wa serikali na chama tawala vilivifunika vile vichache vya kujitegemea ambavyo vinatoa fursa kwa watu wote.

Matatizo ya utoaji habari usio wa haki yalielezewa kuwa na uhusiano wa karibu na kukosa usahihi. Washiriki walisema kwamba waandishi wa habari mara nyingi hawakuakisi vichwa vya habari na zinakuwa na majina ambayo yamekosewa tahajia na taarifa zisizo sahihi. Mshiriki mmoja alisema kwamba ilikuwa kawaida, mathalan, kwa mwandishi wa habari kutoa maelezo yanayotofautiana kuhusu tukio moja ambazo hazichagizwi na ukweli bali na itikadi za kisiasa za waandishi.

Kunukuu vibaya nyanzo vya habari, alisema mshiriki, ilikuwa ni kawaida:

Unaweza kuhojija na waandishi wawili wa habari. Mmoja atatoa maelezo sahihi, lakini mwengine atasema kitu kingine tofauti kabisa na kukihusisha na wewe. Wakati mwengine, maelezo na maoni yanatafsiriwa isiyvo na kupewa mtizamo tofauti kabisa na kile kilichomaanishwa.

Waandishi wa habari walisema viwango duni vinasababishwa na haraka ili kwenda na muda uliowekwa na kukosekana kwa mifumo imara ya udhibiti

kwenye vyumba nya habari. Kuhamia kwenye vyombo vingine nya habari pamoja na kupunguzwa kazi kwa miaka mingi kumepunguza idadi ya waandishi nguli wa habari ambao bado wanajishughulisha na uhandishi wa habari. Mmoja wa washiriki alieleza kwamba kutokana na watu kuwa wachache kwenye vyumba nya habari, ilikuwa ni rahisi kushindwa kuona dosari.

Zamani kulikuwepo na waangalizi. Kwa kawaida, habari zilipitia kwa wahariri wa habari, wahariri wasaidizi, wapitiji, na mpitiaji mkuu na mhariri wa mahudhui kabla ya kuchapishwa. Lakini siku.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria												
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria	✓	✓	✓	✓								
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria		✓			✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria												
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria												

Wastani wa alama:

2.7

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 2.1; 2008: 2.3; 2010: 3.2; 2012: 3.3; 2015: 2.9

4.2 Vyombo nya habari vinifuata maadili ya hiari ya viwango nya weledi, ambavyo vinatiliwa mkazo na vyombo huru visivyo nya kisheria ambavyo vinashughulikia malalamiko kutoka kwa umma

Baraza la Vyombo nya Habari Tanzania (MCT), ambalo ndicho chombo kikuu kinachosimamia maadili ya vyombo nya habari, lina mamlaka-kifani ya kutoa maamuvi. Kwa kawaida, linapokea malalamiko kutoka kwa umma na mara nyingi huyapatia ufumbuzi malalamiko yanayohusiana na vyombo nya habari kabla hayajafika mahakamani.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria												
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria												
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria												
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria						✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓

Wastani wa alama:

4.5

Alama ya miaka iliyopita:

2006: 3.4; 2008: 2.9; 2010: 2.9; 2012: 3.8; 2015: 4.1

4.3 Ngazi za mishahara na mazingira ya jumla ya utendaji kazi, ukiwemo usalama, kwa waandishi wa habari na wanahabari wengine vinatosheleza

Washiriki walikisia kwamba takriban asilimia 80 ya waandishi wa habari Tanzania hawana mikataba ya ajira, na hii ina maana kwamba wanapata ujira mdogo na hawastahili mafao mengi ya kikazi. Hali ni mbaya zaidi kwenye vyombo binafsi vya habari na ya kutisha zaidi kwenye redio za kijamii, ambapo wengi wao, isipokuwa kwa wateule wachache hawana malipo maalum kabisa isipokuwa posho kidogo. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, kiwango cha mshahara cha kuanzia ama hakijabadilika au kimeshuka, huku wengine wakilipwa viwango vya chini hadi chini ya Shilingi za Kitanzania 350,000/= (sawa na Dola za Kimarekani 150). Waandishi wa habari wa kujitegemea ni mionganoni mwa wale wanaolipwa kidogo zaidi, ambapo kwa wastani wanalipwa shilingi 10,000/= za kitanzania (sawa na Dola 4 za Kimarekani) kwa kila habari, ikilinganishwa na waandishi wa habari wa nje ambao hulipwa Dola za Kimarekani takriban 350 kwa kazi kama hiyo.

Washiriki walisema kwamba viwango vidogo vya mshahara wa kuanzia viliakisi kiwango cha mshahara kwa kijana mwenye shahada ya kwanza nchi nzima, ambacho ni wastani wa Shilingi 450,000/= za kitanzania (sawa na Dola 200 za Kimarekani) kwa mwezi. Waandishi nguli wa habari wanapata zaidi ya hapo kidogo. Waandishi wa habari waandamizi, mathalan, wanapata Shilingi za Kitanzania takriban millioni moja (sawa na Dola za Kimarekani 434) kwa mwezi, wakati wahariri wanapata kati ya Shilingi milioni 1.5 na million 5 za Kitanzania (sawa na Doala kati ya 650 na 2,170 za kimarekani) kwa wastani. Nje na mishahara, mazingira ya utendaji kazi ni mabaya kwa ujumla. Sharti la kisheria linalowataka wamiliki wa vyombo vya habari kuwapa wafanyakazi wao kinga ya bima na hifadhi ya jamii mara nyingi inakiukwa. Waandishi wasiolipwa mishahara hawastahili kupewa bima na waandishi wote wa habari kwa ujumla hawana kinga dhidi ya majanga ya kikazi. Washiriki walismulia matukio ya mashambulio ya kimwili (ikiwemo kutekwa) kwa waandishi wa habari, ili kushadidia ukosefu wa kinga na usalama kwenye tasnia hii.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>									
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		<input checked="" type="checkbox"/>		<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>		<input checked="" type="checkbox"/>					
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa yya kiashiria							<input checked="" type="checkbox"/>					
4	Nchi inakidhi vipengele vingi yya kiashiria												
5	Nchi inakidhi vipengele vyote yya kiashiria												

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.8

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2.5; 2012: 1.8; 2015: 2.2

4.4 Waandishi wa habari na wanahabari wengine wamejiunga kwenye vyama vya wafanyakazi na/ au vikundi vya kitaaluma, ambavyo vinawakilisha maslahi yao kikamilifu

Umoja wa Waandishi wa Habari Tanzania haujafanya kazi tangu mwaka 2011 lakini umoja mpya, ambaeo ni Umoja wa Wafanyakazi Waandishi wa Habari Tanzania, ulikuwa ndo kwanza umeanzishwa. Pamoja na hilo, kuna Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo Tanzania, ambacho ni muungano wa radio 35 za kijamii, ambacho kinapigania haki za waandishi wa habari wa radio za kijamii kama sehemu ya malengo yake. Vyama vya wafanyakazi Tanzania vimekuwa dhaifu. Kwa hivyo, vyama vya waandishi wahabari vina tabia ya kuangalia mambo mengine yanayohusu vyombo vya habari kama vile haki za vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza na vivango vya kitaaluma. Kundi hili linajumuisha Muungano wa Klabu za Wanahabari Tanzania, Jukwaa la Wahariri Tanzania, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Chama cha Waandishi wa habari za Michezo Tanzania, Taasisi ya Vyombo vya Habari Tanzania, Baraza la Vyombo vya Habari Tanzania na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika. Washiriki walisema kwamba baadhi ya vyama hutoza ada kubwa ya uanachama ambayo huwakatisha tamaa waandishi wa habari wachanga. Hata hivyo, vyama hivi vimekuwa na nguvu katika kuwakilisha maslahi ya waandishi wa habari. TAMWA inadhaniwa kuwa mojawapo ya vyama vya waandishi wa habari vyenye ushawishi zaidi na mara nyingi hutajwa kama taasisi ya kuigwa.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria				✓				✓		
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		✓	✓			✓	✓	✓		✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vya kiashiria								✓		✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vya kiashiria	✓				✓					
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.3

2006: 2.2; 2008: 2.3; 2010: 2.2; 2012: 2.3; 2015: 2.5

4.5 Waandishi wa Habari na vyombo vyahabari wana uadilifu na si wala rushwa

Uhandishi wa habari wa bahasha ya kahawia, mtindo ambapo waandishi wa habari wanapewa fedha taslimu na vitu vingine ya mkononi ili waipambe taarifa, umeenea sana Tanzania. Kutokana na malipo kiduchu na mazingira mabaya ya utendaji kazi, washiriki walisema kwamba waandishi wa habari walikuwa kwenye hatari ya kupokea rushwa na mara nyingi walipata hisani ya vyanzo vyahabari na wenyeji wa matukio. Tabia hii imekithiri wakati wa chaguzi ambapo viongozi wa kisiasa wanadaiwa kuwahonga waandishi wa habari ili kutangaza kampeni zao.

Wanajopo walielezea aina ndogondogo za rushwa kama vile kukubali kupewa usafiri, kulipiwa hoteli na zawadi nyingine zisizohusisha fedha na kubadilishana na habari. Maslahi mahsus ya mmiliki wa chombo cha habari pia yanaathiri jinsi ya kutangaza habari.

Wanajopo walisema kwamba wafanyabiashara fulani wasingeweza kuandikwa vibaya kwenye baadhi ya vyombo vyahabari kutokana na ukaribu wao na wamiliki wa vyombo vyahabari.

Ni vigumu kumpata mwandishi wa habari atakayeandika kuhusu kashfa inayomhusisha mtoaji mkubwa wa matangazo ya biashara. Kulikuwa na mashtaka mahakamani kuhusu kampuni ya bia kutokana na kuzalisha bidhaa mbovu. Kila wakati chumba cha mahakama kilikuwa kimejaa waandishi wa habari, lakini hakuna habari yoyote iliyandikwa au kutangazwa baada ya hapo. Vyombo vyahabari havitatangaza ajali inayohusisha kampuni fulani za usafirishaji. Watoaji wakubwa wa matangazo ya biashara wana namna yao ya kuvinyamazisha vyombo vyahabari.

Mashirika machache yana sera inayowataka waandishi wa habari kusema zawadi na mambo mengine wanayopewa na watoa habari. ‘Lakini mara nyingi watasema tu, “Acha hili liwe siri yetu,”’ alisema mmoja wa washiriki.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria						✓		✓	✓	✓
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vyahabari	✓	✓	✓	✓	✓					
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa vyahabari							✓	✓		✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi vyahabari										
5	Nchi inakidhi vipengele vyote vyahabari										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.9

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 2; 2012: 1.5; 2015: 2.3

4.6 Waandishi na wahariri wote hawajichuji

Kwa mujibu wa wanajopo, mtindo wa makala na taarifa ya habari umebadilika miaka mingi kadri waandishi wa habari wanavyotambua uwezekano wa kisasi kutokana na kazi zao. Baada ya kufungiwa mara mbili, wanajopo walisema kwamba waliona mabadiliko ya mtindo wa kampuni ya Mwananchi Communications, ambayo huchapisha gazeti la *The Citizen* na gazeti dada linalotumia lugha ya Kiswahili la *Mwananchi*, ambalo linasifika kwa kuandika taarifa makini. Kujichuja kumekithiri. ‘Kuna habari ambazo sitazisogelea kwa namna yoyote ile,’ alisema mwandishi mmoja wa habari kwenye jopo. ‘Baadhi ya watu wametoweka.’

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria	<input checked="" type="checkbox"/>				<input checked="" type="checkbox"/>			<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu vya kiashiria		<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>				<input checked="" type="checkbox"/>			<input checked="" type="checkbox"/>
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria			<input checked="" type="checkbox"/>		<input checked="" type="checkbox"/>	<input checked="" type="checkbox"/>				
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria										
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria										

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

1.8

2006: 2.1; 2008: 2; 2010: 1.5; 2012: 1.8; 2015: 2.3

4.7 Waandishi wa habari wana vyuo vinavyotoa mafunzo rasmi pamoja na fursa ya kuinua viwango vyao

Kuna fursa nyingi za mafunzo ya uandishi wa habari Tanzania. Baadhi ya vyuo vikuu vinavyotoa mafunzo ya uandishi wa habari ni pamoja na : Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine Tanzania, Chuo Kikuu cha Tumaini (Dar es Salaam na Iringa), Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mbali na vyuo vikuu, idadi kubwa ya vyuo vinatoa mafunzo ya uandishi wa habari kwa ngazi ya Stashahada na cheti. Hata hivyo, wanajopo walisema kwamba ubora wa mafunzo wanayopata wanafunzi unahitaji kuboreshwa. Ilielezwa kwamba wahadhiri wengi wa vyuo vikuu hawajawahi kufanya kazi ya uandishi wa habari na hivyo hawana usoefu katika kuandika habari na kutafuta habari.

Fursa nyingine zinapatikana nje ya mfumo wa elimu. *Daily News*, ambalo ni gazeti linalomilikiwa na serikali, mara nyingi huwapeleka waandishi wa habari nchini China, shukrani kwa ubia na serikali ya China. Mashirika kama vile UNESCO yamekuwa yakijihuisha na mafunzo na kuwezesha redio za kijamii na yamejenga ushirikiano na na vyuo nya uandishi wa habari kutengeneza mfumo wa kujifunza kielektroniki. Washiriki wengine wakuu ni pamoja na BBC Media Action, ambayo

inajihusisha na ukuzaji wa vyombo nya habari Tanzania. Wanajopo walisema kwamba mafunzo yanayofadhiliwa na wahisani yana chanagoto zake kwa kuwa mara nyingi huwa na wigo mdogo na huwalenga waandishi wale wale.

Mafunzo ya ndani na uwezeshaji pia yanapatikana lakini mara nyingi hayaratibivi vizuri.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria											
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria											
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria	✓	✓		✓		✓	✓	✓	✓	✓	
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria		✓	✓	✓	✓	✓	✓	✓			
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria											✓

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

3.6

2006: 3.2; 2008: 2.3; 2010: 3.3; 2012: 3.7; 2015: 3.9

4.8 Fursa sawa bila kujali asili au ukabila, tabaka, jinsia, dini na umri unakuzwa kwenye vyombo nya habari

Vyombo nya habari Tanzania vinaakisi mchanganyiko na mgawanyiko wa jamii kwa upana wake. Kwa mujibu wa wanajopo, sekti ya habari ina unyanyasaji wa kingono na ubaguzi wa kijinsia usio wazi. Pamoja na hatua nzuri katika kukuza usawa wa kijinsia, wanawake wangali wanawakilisha asilimia kiduchu ya uongozi wa juu kwenye vyombo nya habari nya umma na vile nya binafsi. Katika sekti nzima, ni wamiliki wawili tu wa vyombo nya habari na wasimamizi wawili ambaeo ni wanawake, isipokuwa kwa redio za kijamii ambapo wamiliki watano kati ya 35 ni wanawake.

Wanajopo walieleza kwamba unyanyasaji wa kingono ni tatizo kubwa kwenye vyombo nya habari nya Tanzania:

Kumekuwepo na malalamiko lukuki ya 'rushwa ya ngono.' Wahariri wa kiume mara nyingi huomba rushwa ya ngono kutoka kwa waandishi wa habari wanawake ili tu taarifa zao za habari zipate kuandikwa. Wakati mwagine hupanga safari na waandishi wa habari wanawake kwa matumaini ya kufanya nao ngono. Wahanga wa tabia hii ni pamoja na wanafunzi waliopo kwenye mafunzo kwa vitendo.

Sheria za Tanzania huchukulia ngono iliofanyika kwa sababu ya madaraka ya mtu kama ubakaji. Mtuhumiwa akikutwa na hatia, anaweza kufungwa hadi miaka 30 jela. Lakini hii hajaweweza kuzuia tabia hii.

Aidha, wanajopo walisema kwamba ubaguzi wa umri ulikuwa unashika kasi. Kwa sasa kuna upendeleo wa waandishi wa habari vijana zaidi kwenye vyumba

nya habari. Katika matukio machache, waombaji kazi wameambiwa kwenye mahojiano kwamba walikuwa na umri mkubwa sana kwa kazi hiyo. Moja ya sababu ni mabadiliko ya mandhari ya vyombo nya habari ambayo yamesababisha mahitaji wa waandishi wa habari wenye ujuzi wa teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, wanajopo walisema bado kulikuwa na fursa kwa 'walinzi wazee' ambao 'mara zote wanapatia mambo'.

Ubaguzi unaohusisha imani na ukabila unaonekana zaidi kwenye vituo nya redio za kidini, ambazo huajiri waumini wao. Wanajopo walisema kwamba hakukuwa na wanawake wenye hijabu kwenye vituo nya luninga na wanawake ambao wamekuwa wakiomba kuvaa hijabu wamelazimika kuhamia kwenye vituo nya redio. 'Hakuna taswira halisi ya Tanzania kwenye vyombo nya habari.'

Tanzania haitambui haki ya mahusiano na uhuru wa kutobaguliwa kwa sababu ya tabia za kimahusiano. Kimsingi, mahusiano ya jinsia moja ni kinyume na sheria. Wapenzi wa jinsia moja na LGBTQIA+ nchini kwa ujumla mara nydingi wamekuwa wakibughudhiwa, na kukamatwa. Wanajopo walisema kwamba kulikuwa na mashoga wanaojulikana kabisa kwenye vyombo nya habari.

Alama:

Alama za mshiriki mmoja mmoja:

1	Nchi inakidhi kiashiria								
2	Nchi inakidhi vipengele vichache tu nya kiashiria			✓	✓			✓	✓
3	Nchi inakidhi vipengele kadhaa nya kiashiria	✓	✓	✓		✓	✓		✓
4	Nchi inakidhi vipengele vingi nya kiashiria								
5	Nchi inakidhi vipengele vyote nya kiashiria								

Wastani wa alama:

Alama ya miaka iliyopita:

2.7

2006: n/a; 2008: n/a; 2010: 3.5; 2012: 4; 2015: 3.5

Jumla ya alama kwenye sekta 4:


2.7




GRAFU KULINGANISHA

ENEO LA 1:

Uhuru wa kujieleza, ukiwemo uhuru wa vyombo vya habari, unalindwa na kukuzwa kikamilifu


**ENEO LA 2:**

Mandhari vyombo vya habari, pamoja na vyombo vipyta vya habari, inaonesha mtawanyiko, uhuru na uendelevu




ENEO LA 3:


Sheria ya matangazo ni wazi na huru; vyombo vya umma vimebadilishwa na kuwa vyombo halisi vya umma

**ENEO LA 4:**

Vyombo vya habari vina viwango vya juu vya weledi



ALL ENEO LAS: ULINGANISHAJI AINA ZA AJILI





NINA KIFANYIKE

1. Miaka mitatu hadi minne iliyopita, kulikuwa na mabadiliko gani kwenye mazingira ya vyombo vya habari?

Mabadiliko Chanya

- Kuongezeka kwa idadi ya vyombo vya habari kulikoambatana na kupanuka kwa mitandao ya kijamii kumezuia jaribio la mamlaka kufunga majukwaa ya kujieleza kwa uhuru.
- Fursa zaidi za mafunzo yanayoju muisha wadau wapya zimeibuka katika kipindi cha miaka michache iliyopita, na hivyo kuwapa waandishi wa habari wigo mpana zaidi wa kufanya maamuzi.
- Vyama vya waandishi wa habari vimekuwa imara zaidi katika kuvilinda vyombo vya habari dhidi ya madhila mbalimbali ya vyombo vya habari na uhuru wa uandishi wa habari.

Mabadiliko Hasi

- Fursa za kisiasa na vyombo vya habari zinasinyaa, hasa kutokana na kuanzishwa kwa sheria kandamizi tangu mwaka 2015.
- Ongezeko la matumizi ya wataalam wapotoshaji kwenye mitandao ya kijamii ili kudhibiti uhuru wa kujieleza kumesababisha athari mbaya, na hivyo kuzuia uhuru wa kujieleza.
- Wanawake wamezidi kuwa na taswira hasi mbele ya viongozi waandamizi wa serikali na kwenye vyombo vya habari.
- Imekuwa ni vigumu sana kupata vyanzo vya habari, hususan kutoka kwenye ofisi za umma.

2. Ni jitihada gani zinahitajika katika kipindi cha miaka mitatu hadi minne ijayo?

- Kuna haja ya kuwa na mikakati ya kisheria na ushawishi dhidi ya sheria kandamizi, na harakati hizi zinaweza kuongozwa na CORI.
- Kuna haja ya kuongeza mafunzo kuhusu usalama wa vyombo vya habari na mchanganyiko, na harakati hizi zinaweza kuongozwa na UNESCO/TMF/MCT/THRDC.
- Kuna haja ya kundelea kufanya ushawishi kwa ajili ya kufufua vyama vya wafanyakazi wa vyombo vya habari na kuungana na Shirikisho la Kimataifa la Waandishi wa Habari.
- Kuna haja ya makampuni ya vyombo vya habari kufanya jitihada za maksudi kwa minajili ya kurasimisha mafunzo na kutengeneza fursa zaidi za mafunzo kwenye maudhui yanayowalenga watu wenye ulemavu, jinsia na haki za binadamu.

Wanajopo/washiriki:

Vyombo vya habari:

1. Mwandishi wa Habari na Mtayarishaji wa Vipindi Redioni
2. Mmiliki wa Blogu
3. Mhadhiri wa Uhandishi wa Habari
4. Mwandishi wa Habari
5. Mwandishi wa Habari
6. Mwandishi wa Habari na Mtetezi wa Haki za Vyombo vya Habari
7. Mhariri

Asasi za Kiraia (orodhesha kwa mtiririko wa jina la ubini):

8. Mwanataaluma
9. Mshauri Elekezi wa Ubunifu, Jinsia na Vipaji
10. Mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi
11. Mwanaharakati wa Haki za Walemavu
12. Mwanasheria wa Haki za Kiraia

Mwandishi (Mtunza kumbukumbu)

Eugene N Nforngwa

Mwendeshaji

Sarah Chiumbu

Friedrich-Ebert-Stiftung (FES)
fesmedia Africa
Windhoek
Namibia
Tel: +264 61 417523
Email: info@fesmedia.org
Website: www.fesmedia-africa.org

Friedrich-Ebert-Stiftung (FES)
P. O. Box 4472
Dar es Salaam
Tanzania
Tel: +255 22 2668575 / 2668786
Website: www.fes-tanzania.org

MISA Tanzania
Kinondoni Mkwajuni (along Kawawa
Road), Dar es Salaam
Tanzania
Tel: +255 22 276 2167
Fax: +255 22 276 2168
Email: misatanzania@gmail.com
Website: tanzania.misa.org

